# BARAKA ZA DUA

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian
Masihi aliyeahidiwa na Imam Mahdi a.s.

Mfasiri,
Sheikh Bakri Abedi Kaluta

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA
TANZANIA

***Baraka Za Dua***

Tafsiri ya Kiswahili ya *Barakātud-Du‘ā*

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza ya Kiurdu: Qadian 1893
Chapa ya Kwanza ya Kiswahili: 2009
Nakala: 2000

Kimeenezwa na:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mnazi mmoja, Dar es Salam.
Simu: +255222110473
Fax: +255222121744

Kimechapwa na:
Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salam, Tanzania
Simu: +255222111031

ISBN: **9987-438-07-6**

# FAHARISI

Dibaji ........................................................................... 7

Mfano wa dua iliyokubaliwa. ................................................ 9

Maoni juu ya kijitabu........................................................ 13

Habari nyingine kumhusu Lekh-Ramu wa Peshawar............ 60

Kwa maamiri na watemi na matajiri wenye uwezo na viongozi wa serikali na wenye vyeo.................................................. 61

Tangazo............................................................................ 68

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ

# Dibaji

Baraka za dua (Barakat ud Dua) kiliandikwa na Sayyidna Ahmad a.s., mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, ili kuondoa matatizo ya Sir Sayyid Ahmad Khan K.C.S.I., mwanachuoni na msomi wa India ambaye hakuamini kukubaliwa maombi na Mwenyezi Mungu. Sayyidna Ahmad a.s. amethibitisha kwamba Mwenyezi Mungu anasikia na anakubali maombi ya waja wake. Aliandika: "Kama Bwana Sayyid hatubu kwa wazo lake hili potofu na anasema kuna uthibitisho gani wa athari za dua, basi mimi nimetumwa kuja kuyaondoa makosa ya aina hiyo. Ninaahidi kwamba nitamjulisha Bwana Sayyid mapema kuhusu kukubalika kwa baadhi ya dua zangu, na siyo tu kumjulisha bali nitazichapisha. Lakini papo hapo Bwana Sayyid pia akiri kuwa baada ya kuthibitika madai yangu ataachana na wazo lake hili potofu." Uk. 24

Katika sehemu ya pili, Sayyidna Ahmad a.s. aliandika kanuni saba za kufasiri Kurani Tukufu. Vile vile amethibitisha ukweli wa Islam na Kurani Tukufu kuwa Neno la Mungu kwa hoja zilizo wazi.

Kitabu hiki kilifasiriwa na Sheikh Bakri Abedi Kaluta, mbashiri wa Tanzania. Kisha Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq aliboresha tafsiri hii na kulinganisha na matini ya

Kiurdu. Pamoja naye Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani na Sheikh Mubarak Mahmud pia walishugulikia kazi hii. Vile vile Muhammad Shafiq Sehgal na Sharifu Tanwir Mujtaba walisaidia kwa njia mbali mbali. Tafsiri hii ni tunda la 'Deski ya Kiswahili'

Wote walioshiriki kukamilisha kazi hii nzuri wanastahili kuombewa. Mwenyezi Mungu Awabariki na Awajaalie malipo bora na Akubali juhudi na huduma yao, na mafundisho haya yalete athari kubwa katika mioyo ya wasomaji. Amin.

Chaudhri Muhammad Ali M.A.,
Wakilut-Tasnif
Tahrik e Jadid,
Rabwah Pakistan.
26/12/2008

## **Mfano wa dua iliyokubaliwa.**

## *Anise Hind*, Merath

## na shutuma dhidi ya bishara yetu

Nimepokea toleo la gazeti hili la tarehe 25 Machi, 1893 ambamo mna baadhi ya shutuma dhidi ya ile bishara yangu niliyoichapisha kumhusu Lekh-Ramu wa Peshawar, na nimefahamu kuwa hata baadhi ya magazeti mengine pia yamesumbuliwa na neno hili la haki. Kwa hakika ni jambo la furaha kwangu kwamba kwa njia hii bishara hii inapata kujulikana na kuenea kwa mikono ya wapinzani wenyewe. Basi mimi kwa wakati huu, katika kuijibu shutuma hiyo, ninaona inatosha tu kuandika kuwa Mwenyezi Mungu namna Alivyotaka ndivyo alivyotenda; mimi simo humo. Naam, suala hili kwamba bishara ya aina hii haitakuwa na faida na ndani yake shaka zitabaki, kuhusiana na shutuma hii nafahamu vema kuwa hiyo ni papara tu kabla ya wakati wake. Mimi nilikiri jambo hili na hata sasa nalikiri kwamba ikiwa, kama walivyofikiri watoa shutuma, hatimaye matokeo ya utabiri huo yawe kwamba huyo akapata homa ya kawaida au maumivu kidogo au akashikwa na kipindupindu na halafu hali ya asili ya afya (yake) ikarejea, basi hiyo haitahesabika kuwa ni kutimia kwa bishara, na bila shaka hiyo itakuwa ni hila na uadanganyifu. Kwani hakuna yeyote aliyeepukana na maradhi ya aina hii; sisi sote wakati fulani tunaumwa. Hivyo, kwa hali hii bila shaka nitakuwa mwenye kustahili

adhabu ile niliyoitaja. Lakini kama bishara ikitimia kwa namna ambavyo ndani yake alama za adhabu ya Mwenyezi Mungu zionekane wazi wazi kabisa, basi hapo mtambue kuwa bishara hiyo imetoka kwa Mwenyezi Mungu. Hakika yenyewe ni kwamba taadhima na hofu ya bishara haihitaji kuwekewa siku na nyakati. Kuhusu habari hiyo inatosha tu kuweka muda maalum kwa zama za kushuka adhabu. Halafu kama kwa hakika bishara idhihiri kwa matisho makubwa, basi yenyewe huivutia mioyo, na mawazo yote haya na shutuma zote hizi zizalikazo nyoyoni kabla ya kutimia kwa bishara hutoweka kabisa hata kwamba waadilifu wenye busara wanaachana na rai zao wakitahayari. Mbali na hayo, mimi pia nipo chini ya kanuni ya maumbile. Ikiwa msingi wangu wa bishara hii uwe tu kwamba mimi nimeitangaza bishara hii kwa kupayuka na kufikiria maradhi kadha anayoweza kupata kwa kubahatisha, basi yule mtu ambaye bishara hii inamhusu, yeye naye anaweza kufanya hivyo hivyo na kutoa bishara kunihusu mimi kwa kubahatisha hivyo. Bali mimi niko radhi kwamba badala ya miaka sita ambayo ni muhula niliomwekea, aandike miaka kumi kwa ajili yangu. Umri wa Lekh-Ramu kwa wakati huu, pengine kwa wingi kabisa ni miaka thelathini, naye ni mtu aliye kijana mwenye umbo lenye nguvu na afya bora; na mimi umri wangu kwa wakati huu ni zaidi ya miaka hamsini, tena ni dhaifu na mwenye kusumbuliwa daima na maradhi, na ninaugua kwa

maradhi mbalimbali; lakini hata hivyo katika mashindano hayo itajulikana kauli ipi imetoka kwa mwanadamu na kauli ipi imetoka kwa Mwenyezi Mungu. Na kauli ya mtoa shutuma kwamba hizi si zama za bishara za aina hii, ni sentensi ya kawaida tu ambayo watu wengi huitamka vinywani mwao. Nifikirivyo mimi, hizi ni zama za kukubali kweli zilizo imara na kamilifu ambazo pengine mfano wake hauwezi kupatikana katika zama zilizopita. Naam, katika zama hizi udanganyifu wowote na hila yoyote haiwezi kufichika; lakini hili ni jambo la furaha zaidi kwa wakweli, kwa sababu yule mtu ajuaye kutofautisha udanganyifu na ukweli ndiye huyo mwenye kuuheshimu ukweli kwa moyo kwa furaha hukimbilia kuukubali ukweli. Na ndani ya ukweli kuna mvuto ambao unamfanya mtu aukubali. Ni dhahiri kwamba zama hizi zinaendelea kuyakubali mamia ya mambo ambayo hayakukubaliwa na mababu wa watu wa zama hizi. Kama zama hizi hazina kiu ya ukweli, kwa nini mapinduzi makubwa yameanza ndani yake? Bila shaka hizi zama ni rafiki wa kweli zilizo halisi, sio adui. Na kusema kwamba zama zina akili na wakati wa watu wasiojua mengi umeshapita, hii kwa maneno mengine ni sawa sawa na kuzikejeli zama hizi; kana kwamba zama hizi ni mbaya kiasi hiki kwamba baada ya kuukuta ukweli kuwa ukweli hasa, hata hivyo haziukubali. Lakini mimi kamwe sitokubali kwamba kweli iko hivyo, kwani mimi naona kuwa wengi wanaonijia na kufaidika nami ni wale wale

walioelimika ambao baadhi yao wamefika hadi shahada ya B.A. na M.A. Na pia ninaona kwamba kundi hili la walioelimika huwa wanaupokea ukweli kwa shauku sana. Na si hivyo tu, bali kundi moja la Waislamu wapya, Wazungu walio na baba au mama wa Kihindi walioelimika waishio maeneo ya Madras wamejiunga katika Jumuiya yetu na wana yakini juu ya kweli zote. Sasa nadhani nimeshayaandika mambo yote yale yanayotosheleza kumfahamisha mtu amchaye Mungu. Wa-Ariya wanayo hiari ya kuyaeleza madhumuni yangu haya wapendavyo; silijali hilo, kwa sababu ninafahamu kwamba kwa wakati huu kuisifu bishara hii au kuiponda yote ni sawa tu. Ikiwa hii imetoka kwa Mwenyezi Mungu, nami nafahamu kabisa kwamba imetoka Kwake, basi lazima itatimia kwa ishara yenye kutisha na kuitetemesha mioyo. Na kama haikutoka Kwake, basi itadhihirika dhila yangu; na kama wakati huo nitatoa taawili mbovu, basi hiyo itasababisha kunidhalilisha zaidi. Yule Dhati wa tokea azali, Mtukufu na Mtakatifu, Ambaye Anayo mikononi Mwake madaraka yote, Hampi mwongo heshima. Si sahihi kabisa kwamba mimi nina uadui binafsi na Lekh-Ramu. Mimi sina uadui binafsi na mtu yeyote yule; bali mtu huyu aliuadui ukweli na akamtaja kwa kumkashifu yule Mkamilifu na Mtakatifu aliyekuwa chemchemi ya kweli zote. Ndiyo sababu Mwenyezi Mungu akataka kudhihirisha duniani heshima ya mpendwa wake. Na amani iwe juu ya yule aufuataye mwongozo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ [1]

نَحْمَدُهٗ وَ نُصَلِّى عَلٰى رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ [2]

# Maoni juu ya kijitabu

***'Addua walistijabah'*** na kijitabu ***'Tahrir fi Usulit-Tafsiri'***

vya Sayyid Ahmad Khan, K.C.S.I.

(Tafsiri ya beti za Kiajemi):

*Ee mfungwa wa akili yako, usione fahari juu ya dhati yako;*
*kwani mbingu hii ya ajabu huleta watu wengi kama wewe.*
*Asiyehusika hana nafasi ya kupita mtaani mwa Mungu;*
*Yule ajaye toka mbinguni ndiye aletaye siri ya rafiki yake.*
*Mtu kuelewa mwenyewe Kurani ni wazo batili;*
*Yeyote atoaye maelezo kwa rai yake mwenyewe,*
*anatoa uchafu na nyamafu.*

---

1 Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

2 Tunamhimidia Yeye na tunamsalia Mtume Wake Mtukufu s.a.w.

Bwana Sayyid katika kijitabu chake kilichotajwa katika kichwa cha maneno anadhihirisha itikadi yake kuhusiana na dua kwamba maombi kukubaliwa hakuna maana kwamba kiombwacho katika dua, mtu apewe hicho. Kwani kama maana ya kukubaliwa maombi ndiyo hii tu kwamba kiombwacho kitimizwe kwa vyo vyote, hapo matatizo mawili yanajitokeza. Kwanza ni kwamba maelfu ya dua yanaombwa kwa unyenyekevu na kiherehere lakini ombi halitimii, ambayo humaanisha kwamba dua haikukubaliwa ilhali Mwenyezi Mungu Ameahidi kukubali maombi. Pili ni kwamba yale mambo yatakayotokea yamekwisha kadiriwa, na yale ambayo hayatatokea nayo yameshakadiriwa; haiwezekani kamwe kutokea kinyume na yaliyokadiriwa tayari. Basi kama maana ya kukubaliwa dua ichukuliwe kuwa ni kutimia ombi, hapo ahadi hii ya Mwenyezi Mungu

اُدْعُوْنِیْٓ اَسْتَجِبْ لَكُمْ[3]

haiwezi kuhusika na yale maombi yaliyokadiriwa kutotimia. Yaani, sawa na maana hizi, ahadi hii inayohusikana na maombi yote kukubaliwa itabatilika, kwani sehemu ile ya maombi yatimizwa ambayo kutimia kwake kumekadiriwa. Lakini ahadi ya kukubaliwa dua ni kuzihusu dua zote pasipo

[3] Niombeni Nitawajibuni. Al-Mu’min : 61

kuiacha dua yoyote. Hivyo, ikiwa baadhi ya aya zinadhihirisha kwamba vile vitu ambavyo havikukadiriwa kupewa havitopewa kamwe ambapo kutokana na baadhi ya aya inathibitika kwamba hakuna dua yoyote inayokataliwa, bali zote zinakubaliwa, na siyo hiyo tu bali inathibitika pia kwamba Mwenyezi Mungu Amekwisha ahidi kuzikubali dua zote kama inavyodhihirika kwa aya ya

اُدۡعُوۡنِیۡۤ اَسۡتَجِبۡ لَکُمۡ ؕ

Hivyo, ukinzani na hitilafu baina ya aya hizo yawezaje kuepukika isipokuwa kama maana ya kupokelewa dua ichukuliwe kumaanisha kukubalika kwa ibada. Yaani, ichukuliwe maana hii kwamba dua ni ibada, na Mwenyezi Mungu Ameahidi kuikubali hiyo kama ikifanywa kwa moyo, unyeyekevu na kujidhalilisha. Basi, muradi wa kukubalika dua si mwingine isipokuwa kwamba dua hiyo yahesabiwa kuwa ibada na thawabu hupewa kwayo. Naam, ikiwa ndani ya takdiri imekadiriwa kukipata kitu fulani na kwa bahati dua nayo ikaombwa kwa ajili yake, basi kitu hicho hupatikana; lakini siyo kwa sababu ya dua bali kupatikana kwake kulikwisha kadiriwa. Na faida kubwa ya kuomba dua ni hii kwamba wakati wa kuomba dua inapofikiriwa sana mno moyoni taadhima na kudra isiyo na kikomo ya Mwenyezi Mungu, hapo fikira hiyo huja kuyashinda mawazo

yote yale yaliyosababisha mahangaiko na mtu hupata subira na uimara. Na kuzalika kwa hali ya aina hii moyoni ni hali ya lazima ya ibada, na hiyo ndiyo kukubaliwa kwa dua. Tena Bwana Sayyid anaandika mwishoni mwa kijitabu chake kwamba wale watu wasioufahamu uhakika wa dua na wasiotambua hekima iliyomo ndani yake, wanaweza kusema kwamba iwapo jambo hili limeshakubaliwa kuwa lisilokadiriwa kutokea, haliwezi kutokea, basi dua yafaa nini? Yaani, kama lililokadiriwa kupewa mtapewa tu, mkiomba au msiombe, na lile lisilokadiriwa kutolewa hata mkiliombea maelfu ya dua haitafaa kitu, basi hapo kuomba dua ni bure. Kwa kulijibu, Bwana Sayyid anasema kwamba wakati wa mahangaiko kutamani kuomba msaada ndiyo tabia ya asili ya mwanadamu; hivyo mwanadamu huomba dua kwa sababu ya tabia yake ya asili bila kufikiria kuwa jambo hilo litatukia au la. Na sawa na tabia yake ya asili akaambiwa kwamba Muombe Mungu tu chochote uombacho.

Kwa maandiko yote hayo ambayo tumeyaandika kwa muhtasari hapo juu yamethibitika kuwa itikadi ya Bwana Sayyid ni kwamba dua haiwezi kuwa njia ya kupatia kusudio na wala haina athari yoyote katika kuyapata makusudio. Na kama katika kuomba dua kusudio la mwenye kuomba ni hili tu kwamba haja

yake fulani itimie kwa sababu ya kuomba, basi wazo hili ni bure tu, kwani jambo lililokadiriwa kutokea halihitaji dua, na lile lisilokadiriwa kutokea kuliombea dua kwa unyenyekevu hakuna faida. Ilmuradi, kwa maneno hayo bayana imedhihirika kwa uwazi kabisa kuwa itikadi ya Bwana Sayyid ni hii hii kwamba shabaha ya dua ni ibada pekee, na kuihesabu kuwa njia ya kupatia kusudio lolote la kidunia ni tamaa isiyo sahihi.

Sasa ibainike kwamba Bwana Sayyid amepata kudanganyika sana katika kuzielewa aya za Kurani Tukufu; lakini inshallah tutaibainisha hali ya kudanganyika huko mwishoni mwa madhumuni haya. Wakati huu twadhihirisha kwa masikitiko makubwa kwamba kama Bwana Sayyid hakuwa na ufahamu mkubwa wa kuielewa Kurani Tukufu, je hata kanuni ya maumbile, ambayo anadai kuifuata na ambayo anaidaia kuwa mwongozo wa Mwenyezi Mungu kwa kitendo na kuwa mfasiri wa siri zilizofichika za Kurani Tukufu, hakuiona wakati aandikapo madhumuni haya? Je, Bwana Sayyid hafahamu kuwa ingawa hakuna shari au heri yoyote ya dunia isiyokuwa imekadiriwa, hata hivyo kanuni ya maumbile imeiwekea sababu za kuipata ambazo athari zake sahihi na za kweli hakuna mwenye akili anayezikataa. Kwa mfano, ingawa kwa sababu ya

takdiri, kutumia dawa au kutoitumia kwa hakika ni sawa sawa na kuomba dua au kutoomba, lakini je Bwana Sayyid anaweza kuwa na maoni kwamba, mathalan, elimu ya utabibu ni batili kabisa, na Mwenye Hekima wa kweli Hakuweka athari yoyote katika dawa? Tena, ikiwa Bwana Sayyid, juu ya kuiamini takdiri, analikiri pia jambo hili kwamba dawa vile vile hazijakosa athari (ya kutibu), basi kwa nini analeta tofauti na utengano katika kanuni ya Mwenyezi Mungu iliyo sawa na hiyo na yenye kushabihiana nayo? Je imani ya Bwana Sayyid ndiyo kwamba Mwenyezi Mungu Alikuwa na uwezo wa kuweka athari kali ndani ya turbad (mzizi fulani iliyo haluli), sakmunia (gundi fulani iliyo haluli kali), sanamaki na habbulmuluki (mbegu fulani), kwamba kwa kutumia tu dozi kamili ya hizo mtu aanze mara moja kuharisha. Au kwa mfano katika aseniki na akonaiti na katika sumu zingine zenye kuangamiza atie athari kali sana kwamba dozi timilifu ya hizo imfanye ainywaye kuaga dunia katika dakika chache, lakini dua za waja wake ziombwazo kwa mwelekeo, hima na unyeyekevu Aziache kama mfile zisizokuwa na athari hata chembe ndani yake? Je, inawezekana kwamba kuwe na hitilafu ndani ya nidhamu ya Mwenyezi Mungu, na Aliyokusudia katika dawa kwa ajili ya manufaa ya waja wake yasizingatiwe katika maombi? Hapana, hapana; la hasha! Bali, Bwana

Sayyid mwenyewe hana habari ya falsafa ya kweli ya maombi wala hana uzoefu binafsi wa athari zake kubwa. Mfano wake ni kama wa yule atumiaye kwa muda mrefu dawa fulani iliyokwisha muda wake na kupoteza nguvu zake na kwa kuiona haina athari yoyote ile, aiamulie kwa jumla dawa yenyewe hiyo kwamba haina athari yoyote. Ni masikitiko, tena masikitiko mengi mno kwamba ingawa Bwana Sayyid amekwisha kuwa mzee lakini hadi sasa kawaida hii ya nidhamu ya takdiri imefichika kwake kwamba takdiri imefunganishwaje na sababu, na ni namna gani kawaida ya sababu na matokeo ina uhusiano mkubwa na wa lazima ndani kwa ndani, na ndiyo sababu akapata kudanganyika na akadhani kuwa bila ya sababu ambazo kanuni ya maumbile imeziweka kwa njia ya kiroho na kiwiliwili kitu chochote chaweza kutokea. Kweli hakuna kitu chochote duniani kisicho chini ya takdiri; kwa mfano, mtu anafaidika na moto, maji, hewa, udongo, nafaka, mimea, wanyama, madini na kadhalika, hivyo vyote kwa hakika vimekadiriwa; lakini kama asiye na elimu adhani kuwa bila ya sababu zote zile Alizoziweka Mwenyezi Mungu na bila ya njia ambazo kanuni ya maumbile imeziweka, kitu fulani chaweza kupatikana bila ya kupitia njia za kiroho au za kimwili, basi mtu huyo kana kwamba anataka kuibatilisha hekima ya Mwenyezi Mungu. Mimi sioni kwamba maelezo ya

Bwana Sayyid yanamaanisha lolote isipokuwa kwamba yeye haifahamu dua kuwa ni miongoni mwa sababu ziletazo matokeo anazokubali kwa imara bali ametambuka mipaka katika njia hii. Kwa mfano, kama Bwana Sayyid aelezwe athari ya moto hataikataa, na kamwe hatasema kwamba kama imekadiriwa kwa fulani kuungua basi ataungua tu hata bila ya moto. Basi hapo nashangaa kwamba juu ya yeye kuwa Mwislamu, kwa nini anazikataa athari za dua amabzo kama moto pengine zaangaza gizani na pengine zaunguza mkono wa mtovu wa adabu aingiliaye kati. Je, yeye anakumbuka takdiri wakati wa dua tu, na utajwapo moto na kadhalika anaisahau takdiri? Je, takdiri hiyo moja haijumuishi vitu vyote hivyo viwili? Tena, kama juu ya kuiamini takdiri, anaziamini kwa nguvu sana sababu zinazoathiri hata kwamba amepata jina baya kwa kupita kiasi katika habari hii. Basi kuna sababu gani kwamba ile nidhamu ya asili ambayo ameshaikiri hakuikumbuka kuhusu dua, hata kwamba nzi ana athari kidogo lakini dua haina hata kiasi hicho. Hivyo ukweli hasa ni huu kwamba yeye hana habari ya uwanja huu na wala hana uzoefu binafsi na wala hakai na wenye uzoefu.

Sasa kwa ajili ya faida ya wote tunadhihirisha uhakika kidogo wa kukubaliwa kwa dua. Basi ibainike kwamba suala la kukubalika dua kwa hakika

ni kitawi cha suala la dua. Na ni jambo la msingi kwamba yule mtu ambaye hakulifahamu shina, yeye hupata matatizo katika kulifahamu tawi na kudanganyika. Basi hiyo ndiyo sababu ya ufahamu potofu wa Bwana Sayyid. Na uhakika wa dua ni huu kwamba kunakuwepo na uhusiano wenye mvuto kati ya mja mwema na Mola Wake. Yaani, kwanza rehema ya Mwenyezi Mungu humvutia mja upande Wake, halafu kwa mivuto ya ukweli wa mja Mwenyezi Mungu Humkurubia yeye. Na uhusiano huo katika hali ya kuomba dua ukifikia mahali maalum, huzalisha sifa za ajabu. Hivyo, wakati mtu akikumbwa na tatizo zito anaelekea kwa Mwenyezi Mungu kwa yakini kamili, matumaini kamili, mapenzi kamili, uaminifu kamili na hima kamili na huku akiwa macho kabisa akiyachana mapazia ya mghafala huendelea mbele zaidi na zaidi katika nyanja za fanaa (kujihilikisha ndani ya Mwenyezi Mungu). Lo! mbele anakuta Baraza la Mwenyezi Mungu, na kwamba hakuna mshiriki yeyote pamoja Naye. Ndipo roho yake inaweka kichwa juu ya kizingiti hicho na nguvu ya kuvutia iliyowekwa ndani yake inayavutia kwake maelekezo ya Mwenyezi Mungu na hapo ndipo Mwenyezi Mungu Mwenye Shani Anaelekea kwa kuitimiza kazi hiyo, na athari ya dua hiyo Anazitilia sababu zote za asili ambazo kwazo zinazalika sababu zile zilizo muhimu kwa

kupata makusudio haya. Kwa mfano, kama kuna dua ya kuomba mvua, basi baada ya kukubaliwa dua, sababu za asili zilizo muhimu kwa ajili ya mvua zaletwa kutokana na athari ya dua hiyo. Na kama ni kuombea vibaya kwa kuletwa njaa, basi Mungu Mweza huumba sababu zilizo kinyume na hizo. Kwa sababu hii hii, sawa na maoni ya watu wenye kupokea kashfi na waliokamilika imeshathibitika kutokana na tajiriba nyingi kwamba ndani ya dua ya mtu aliyekamilika huzalika nguvu ya kuumba. Yaani kwa idhini ya Mwenyezi Mungu dua hiyo inafanya kazi katika ulimwengu wa chini na wa juu na kuleta elementi na vitu vyote vya angani na mioyo ya watu kwenye ule upande uanaotakiwa kusaidiwa unaokusudiwa. Mifano yake si haba ndani ya vitabu vya Mwenyezi Mungu. Bali uhakika wa baadhi ya aina za miujiza, kwa kweli ni kukubaliwa kwa maombi na maelfu ya miujiza iliyodhihiri kwa manabii au mambo ya maajabu waliyoendelea kuonyesha Mawalii mpaka siku hizi, asili na chimbuko lake ni hii hii dua. Na mara nyingi kwa athari tu ya maombi, miujiza huendelea kuonyesha onyesho la uwezo wa Mweza. Lile tukio la ajabu liliotukia katika nchi ya jangwa la Arabuni kwamba malaki ya wafu wakahuika katika siku chache, na waliokuwa wameharibika tangu vizazi hata vizazi wakazishika khulka za Mungu, na vipofu wakaanza

kuona, na midomo ya mabubu ikaanza kueleza maarifa ya Mwenyezi Mungu, na mara moja mapinduzi yale yakapatikana duniani ambayo hakuna jicho lolote lililoyaona hapo kabla, wala sikio lolote lililoyasikia. Mwafahamu hiyo ilikuwa ni nini? Hizo zilikuwa ni dua za mausiku yenye kiza za mja aliyejipoteza ndani ya Mwenyezi Mungu, ambazo zikapaza vilio duniani na zikaonyesha maajabu yaliyoonekana hayawezekani kwa yule asiye na msaidizi asiyejua kusoma na kuandika. E Mungu, Umrehemu na umpe amani na Umbariki yeye na ali zake kiasi cha hamu yake na ghamu yake na huzuni yake kwa ummati huu, na Umteremshie nuru za rehema Yako hadi milele. Nami pia naona kutokana na tajiriba yangu binafsi pia kuwa athari za maombi ni zaidi kuliko athari za maji na moto, bali katika utaratibu wa sababu za asili hakuna kitu chenye athari kubwa sana kama dua.

Na kama kuna wasiwasi kwamba baadhi ya dua hazikubaliwi na athari zao hazionekani, basi nasema kuwa hali hii ndiyo ya dawa pia. Je  dawa zimefunga mlango wa mauti? Au dawa kushindwa kuathiri ni jambo lisilowezekana? Lakini juu ya yote hayo je, kuna yeyote awezaye kuzikataa athari zake? Ni kweli kwamba takdiri inakizunguka kila kitu, lakini takdiri haikuzipoteza elimu wala kuzidhalilisha na wala

haikuzionyesha sababu (za matukio ya mambo) kuwa hazitegemewi. Bali kama mkitafakari, mtaona kwamba sababu hizi za kimwili na kiroho pia hazipo nje ya takdiri. Kwa mfano, kama takdiri ya mgonjwa fulani ni njema, basi sababu za takdiri ya tiba hupatikana kikamilifu na hali ya mwili pia huwa katika kiwango fulani hata kwamba unakuwa tayari kufaidika nazo. Hapo dawa huathiri kama inavyolengwa shabaha barabara. Na hiyo ndiyo pia kanuni ya dua. Yaani kwa ajili ya dua pia, sababu zote na masharti yote ya kukublika kwake hujumuika pale tu penye dhamiri ya Mwenyezi Mungu ya kukubali. Mwenyezi Mungu Ameifunga nidhamu Yake ya kimwili na kiroho kwenye mfumo ule ule mmoja wa vinavyoathiri na vinavyoathirika. Hivyo, ni kosa kubwa la Bwana Sayyid kwamba aikiri nidhamu ya kimwili lakini akana nidhamu ya kiroho.

Mwishoni, naona ni muhimu kusema kwamba kama Bwana Sayyid hatubu kwa wazo lake hili potofu na anasema kuna uthibitisho gani wa athari za dua, basi mimi nimetumwa kuja kuyaondoa makosa ya aina hiyo. Ninaahidi kwamba nitamjulisha Bwana Sayyid mapema kuhusu kukubalika kwa baadhi ya dua zangu na siyo tu kumjulisha bali nitazichapisha. Lakini papo hapo Bwana Sayyid pia akiri kuwa baada ya kuthibitika madai yangu ataachana na wazo lake hili potofu.

Kauli ya Bwana Sayyid ni kana kwamba ndani ya Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu Ameahidi kuzikubali dua zote ilhali dua zote hazikubaliki; hapo ameelewa vibaya sana. Na aya hii اُدۡعُوۡنِیۡۤ اَسۡتَجِبۡ لَکُمۡ ؕ[4] haziwezi kumsaidia chochote katika shabaha yake, kwani dua iliyoamuriwa ndani ya aya ya 'Ud uni astjib lakum' kuombwa mradi wake sio dua za kawaida, bali ni ibada ile aliyofaradhishiwa mwanadamu, kwani muundo wa amri hapa ni dalili ya kufaradhisha. Na ni dhahiri kwamba dua zote haziingii katika faradhi; bali katika mahali fulani, Mwenyezi Mungu amewasifu wale wenye subira ambao wanatosheka kwa kusema 'Inna lillaah'. Dokezo kubwa kwa dua hiyo kuwa faradhi ni kwamba haikutolewa tu amri ya kuomba, bali kwa kuitaja kwa neno la ibada imeonywa kutolewa adhabu ya Jahanamu katika hali ya kuiasi. Na ni dhahiri kwamba kuhusu dua zingine onyo hilo la adhabu halipo, bali wakati mwingine manabii wamekaripiwa na kukemewa walipoomba, na aya

اِنِّیۡۤ اَعِظُکَ اَنۡ تَکُوۡنَ مِنَ الۡجٰہِلِیۡنَ ﴿۴۷﴾[5]

ndiyo ushahidi juu yake. Inadhihirika wazi kabisa kutokana na hiyo kwamba kama kila dua ingekuwa ni

4 Niombeni Nitawajibuni. Al-Mu'min : 61

5 Mimi nakunasihi usije ukawa miongoni mwa wajinga. Huud : 47

ibada, basi kwa nini Hadhrat Nuhu a.s. angepigwa kiboko cha لَا تَسۡـَٔلۡنِ (usiniombe)? Na wakati mwingine mawalii na manabii wakaona kuomba dua kuwa ni utovu wa adabu, na watawa wakajiuliza moyo fatuwa kuhusu dua za aina hiyo. Yaani kama wakati wa shida moyo umetoa fatuwa ya kuomba dua basi walielekea kuomba dua; na kama moyo ulitoa fatuwa ya kufanya subira basi hapo walifanya subira na kujiepusha na kuomba dua. Isitoshe, Mwenyezi Mungu Hakuahidi kuhusu dua nyingine kuzikubali; bali Amesema kwa uwazi kuwa "Nikipenda Nitazikubali, Nikipenda Nitazikataa", kama isemavyo aya ya Kurani wazi wazi, nayo ndiyo hii:

بَلۡ اِيَّاهُ تَدۡعُوۡنَ فَيَكۡشِفُ مَا تَدۡعُوۡنَ اِلَيۡهِ اِنۡ شَآءَ [6]

Na hata kama tukubali hapa neno "Ud'uu" kikawaida mradi wake ni dua tu, hapo hatuna budi kuamini kuwa hapa dua mradi wake ni ile dua inayoombwa kwa kutimiza masharti yote; na kuyajumuisha masharti yote haimo katika hiyari ya mwanadamu bila kusaidiwa na uwezo aliokwisha jaliwa tangu zamani. Na ikumbukwe pia kuwa unyenyekevu pekee hautoshi katika kuomba dua, bali yahitajika pia Ucha Mungu, utakaso, uongofu, yakini kamili, mapenzi kamili, mwelekeo kamili, na kwamba yule mtu

---

6 Bali Yeye ndiye mtamwita, naye Atawaondoleeni mnayomwitia, Akipenda. Al-Anaam :42

anayejiombea dua au anayeombewa dua kulipata kwake jambo hilo kusiwe pia kinyume na hekima ya Mwenyezi Mungu kwa sababu pengine ndani ya dua masharti yote hujumuika lakini kile kitu kilichoombwa huwa kinyume na hekima ya Mungu katika elimu ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya muombaji na kunakuwa hamna heri katika kukitimiza. Kwa mfano, kama mtoto mpendwa wa mama akimwomba kwa kung'ang'ania na kulia sana kwamba ampe mkononi mwake kipande cha moto au mtoto wa nyoka, au sumu fulani ambayo kwa dhahiri inaonekana nzuri, basi mama yake hatalitimiza kamwe ombi la mtoto huyo; na kama akilitimiza na kwa bahati mtoto amesalimika lakini kiungu chake fulani kimedhurika basi baada ya kubalehe mtoto huyo atalalamika sana kwa mama huyo mpumbavu. Na mbali na hayo, kuna masharti mengi mengine pia ambayo yasipotimia yote hayo dua haiwezi kusemwa kuwa ni dua. Na isipoingia kikamilifu athari ya kiroho ndani ya dua yoyote na usipokuwepo ukaribu kati ya anayeombewa na anayemwombea, kutazamia athari ya dua kudhihiri ni matarajio yasiyotimia, na maadamu Mwenyezi Mungu Asipotaka kupokea dua, masharti yote hayo yanakuwa hayajumuiki, na bidii zinashindwa kupata mwelekeo mkamilifu. Bwana Sayyid analiamini pia jambo hili kwamba wema, neema, ladha na raha za Akhera ambazo humaanisha

wokovu ni matokeo ya imani na dua za kiimani. Na hali ikiwa ndiyo hii, Bwana Sayyid akalazimika kuamini kuwa bila shaka dua za mwaminio zina athari ndani yake na zinakuwa sababu ya kumwondolea maafa na kumpatia makusudio; kwani kama haziwezi kuwa sababu (ya kuondoa maafa na kupata makusudio), kwa nini zitakuwa sababu (ya mambo hayo) kule kiyamani? Jambo hili liko wazi kabisa kuwa ikiwa ndani ya dua, kwa hakika, mna athari yoyote ya kuepuka maafa (ya huko Akhera), basi athari hiyo inapaswa kudhihiri ndani ya dunia hii pia ili yakini yetu izidi na matumaini yetu yaongezeke na ili tuombe dua kwa shauku zaidi kwa kupata wokovu wa Ahkera. Na ikiwa kwa hakika dua si kitu chochote bali yatatokea tu yaliyokwisha andikwa katika takdiri, hapo sawa na kauli ya Bwana Sayyid, kama ni bure kuomba dua kwa kuondoa maafa ya dunia, ndivyo itakavyokuwa bure kuomba dua kwa ajili ya Akhera pia na kuitegemea ni tamaa isiyofaa. Sasa nisingependa kuandika zaidi kuhusu jambo hili, kwa sababu wasomaji waadilifu wanaweza kufahamu kwa kuyasoma kwa makini maelezo yangu hayo kwamba nimekwisha toa uthibitisho wa kutosha kuwa Bwana Sayyid alielewa vibaya. Isitoshe, ikiwa Bwana Sayyid bado haachi kung’ang’ania, basi njia nyingine pia imeandikwa kwa ajili ya kumtimizia hoja; kama yu mtafuta ukweli, hatakengeuka. Na kitabu cha pili

cha Bwana Sayyid kiitwacho 'Tahriir fii Usulit-tafsiir' kinapingana na kupinzana na kitabu chake hiki, kana kwamba Bwana Sayyid aliandika vitabu hivi viwili akiwa katika hali ya mahangaiko; kwani ndani ya kitabu cha 'Istijabati Dua', Bwana Sayyid anaitanguliza takdiri, na anaziona sababu za kawaida kana kwamba hazina maana, na kwa msingi huu huu anakataa kupokelewa kwa dua. Maana, dua ni miongoni mwa sababu za kawaida ambazo manabii zaidi ya laki moja na mamilioni ya mawalii wameendelea kuzitolea ushahidi[7] na mikononi mwa manabii mlikuwa na nini tena zaidi ya dua? Na katika

---

[7] Qutbi Rabbani na Ghauthi Subhani, Sayyid Abdul Qadir Jilani r.a. kadiri alivyoandika ndani ya kitabu chake '*Futuhul Ghaib*' kuhusiana na mwelekeo wa mtu aliyekamilika na athari ya maombi yake kwa tajiriba zake, twayaandika maneno hayo hapa chini pamoja na tafsiri kwa faida ya wote. Kusudio la kuyatoa maandiko haya ni kwamba katika kila fani ushahidi unaokubalika ni wa yule mtu aliye mhakiki katika fani hiyo. Basi, kwa sababu hiyo, yule tu aweza kutambua falsafa ya kukubalika dua aliyekwisha pata uhusiano halisi wa kweli na upendo na Mwenyezi Mungu. Basi kumwuliza Bwana Sayyid Ahmad Khan falsafa hii takatifu ni sawasawa na kumwuliza mganga wa mifugo tiba ya ugonjwa wa mwanadamu. Kama Bwana Sayyid aeleze uhusiano wa serikali fulani na raia zake, hapo hakuna shaka yeye anafaa kwa jambo hili, lakini mambo ya Mwenyezi Mungu wanayajua waja wa Mungu tu. Maneno yenyewe ni haya:

kitabu cha pili, yaonekana kana kwamba Bwana Sayyid haifahamu takdiri kuwa ni kitu chochote, kwani amekwisha sema kwamba vitu vyote vyajitegemea, kana kwamba vitu vyote hivyo vimetoka kwenye mamlaka ya Mwenyezi Mungu na sasa Yeye Hana hiyari yoyote ile ya kuvibadilisha na kuvigeuza, na kana kwamba Uungu wake unaishia katika eneo dogo tu, na kazi zake za kuonyesha

---

فَاجْعَلْ اَنْتَ اَجْمِلَتَكَ وَ اَجْزَائَكَ اَصْنَاماً مَعَ سَائِرِ الْخَلْقِ وَ لَا تُطِعْ شَيْئاً مِّنْ ذَالِكَ وَ لَا تَتَّبِعْهُ جُمْلَةً فَتَكُوْنَ كِبْرِيْتاً اَحْمَرَ فَلَا تَكَادُ تَرَى فَحِيْنَئِذٍ تَكُوْنُ وَارِثَ كُلِّ نَبِيٍّ وَ رَسُوْلٍ وَ بِكَ تُخْتَمُ الْوِلَايَةُ وَ تَنْكَشِفُ الْكُرُوْبُ وَ بِكَ تَسْقِى الْغُيُوْثُ وَ بِكَ تَنْبُتُ الزُّرُوْعُ وَ بِكَ تُدْفَعُ الْبَلَايَا وَ الْمِحَنُ عَنِ الْخَاصِّ وَ الْعَامِّ وَ اَهْلِ الثُّغُوْرِ وَ تُقَلِّبُكَ يَدُ الْقُدْرَةِ وَ يَدْعُوْكَ لِسَانُ الْاَزَلِ وَ تَنْزِلُ مَنَازِلَ مَنْ سَلَفَ مِنْ اُولِى الْعِلْمِ وَ يُرَدُّ عَلَيْكَ التَّكْوِيْنُ وَ خَرْقُ الْعَادَاتِ وَ تُؤْمَنُ عَلَى الْاَسْرَارِ وَ الْعُلُوْمِ اللَّدُنِيَّةِ وَ غَرَائِبِهَا

Tafsiri: Ikiwa unataka kukubalika kwa Mwenyezi Mungu basi uwe na yakini na jambo hili na ufahamu hivi kwamba mikono yako, miguu yako, ulimi wako, macho yako, mwili wako wote na viungo vyako vyote kuwa ni masanamu tu yaliyoko njiani mwako; na miongoni mwa viumbe, vitu vingine vyote pia ni masanamu yaliyoko njiani mwako; watoto wako, mke wako na kila kusudio la kidunia ulitakalo na mali ya kidunia na heshima ya kidunia na staha za kidunia na kuitarajia na kuihofia dunia na kuwategemea Zaid na Bakari au kuhofia kuudhiwa na Khalidi na Walidi, haya yote ni masanamu yaliyoko njiani mwako. Hivyo usiwe mtii wa sanamu lolote kati ya masanamu hayo, na usishughulikie kulifuata

uwezo wake unakuwa haziendelei mbele bali zimebaki nyuma. Na ile hali viliyo nayo vitu hivyo si tena takdiri Yake bali sasa hiyo ndiyo sifa yenyewe makhsus ya vitu hivyo isiyoweza kugeuka wala

---

sana hata ukasahau vingine. Yaani, ulitunze sawa na haki za kisheria na suna za watu wema. Basi kama ukiisha fanya hivyo, wewe utakuwa kama kitu kipatikanacho kwa nadra, daraja lako litanyanyuka mno hata kwamba wewe hutaonekana, na Mwenyezi Mungu Atakufanya uwe mrithi wa Manabii na Mitume Wake; yaani elimu zao, maarifa yao na baraka zao ambazo zilikuwa zimefichikana na kutoweka utajaliwa upya na Uwalii utaishia kwako; yaani hatainuka yeyote baada yako atakayekuwa mkubwa kuliko wewe, na kwa dua zako, bidii zako na baraka zako, huzuni kubwa za watu zitaondolewa na mvua zitanyesha kwa waliokumbwa na njaa na mashamba yatastawi, na mabalaa na shida za kila mtu makhsus na wa kawaida hata masaibu ya wafalme yataondolewa kutokana na mwelekeo wako na dua zako. Na mkono wa kudra utakuwa pamoja nawe; popote utakapoelekea huo, nawe utaelekea huko. Na ulimi wa azali utakuita upande wake, yaani lolote litakalotamkwa na ulimi wako litakuwa limetoka kwa Mwenyezi Mungu na litawekewa baraka. Nawe utapewa daraja la wakweli wote waliopewa elimu kabla yako; na nguvu ya kuumba utajaliwa, yaani dua yako na mwelekeo wako utaleta mabadiliko ulimwenguni; hapo utakapotaka kukiletesha kisichokuwepo au kukitowesha kilichopo basi itakuwa hivyo hivyo, na mambo ya kimiujiza yatadhihirika kwako nawe utajaliwa kujua siri zilizofichika na elimu zitokazo Kwake na maarifa yasiyojulikana kwa wengine ambayo utafahamika kuwekewa amana na kuwa mstahiki.

kubadilika kwa sababu ndani ya maana ya takdiri hiyari ya mwendesha takdiri ni jambo la lazima. Hivyo, ni dhahiri kwamba sifa zile makhsus ambazo Mwenyezi Mungu Hana sasa mamlaka juu yake, yawezaje kusemwa kuwa hizo ni sifa ya Mwenyezi Mungu? Na kama yapo mamlaka, basi bado upo uwezekano wa kuzigeuza. Ilmuradi Bwana Sayyid katika kitabu hiki cha pili ameondolea mbali utawala wa Mwenye Kudra wa kweli kutoka kwenye vitu vyote hata kwamba katika sifa zake haviko tena chini ya mamlaka ya Mmiliki (sawa na kauli ya Bwana Sayyid). Bali haki ambazo Waingereza wamewapatia warithi wa wanaowalimia wenye mashamba, katika kifungu cha tano cha sheria inayowahusu — yaani mmiliki wa ardhi hana uwezo wowote wa kuwaingilia shughuli zao — Bwana Sayyid amevihesabu vitu vyote, kama vile moto na kadhalika, kuwa warithi wa aina hiyo. Bali sheria ya Bwana Sayyid ni kali zaidi kuliko ile ya Waingereza, kwani Waingereza wameweka sura moja (kwa mmiliki wa shamba) kumwondoa mrithi aliyetajwa katika kifungu cha tano, nayo ndiyo kwamba mrithi asipolipa sehemu ya mapato ya mazao hata kama ni Anna[8] mbili tu, basi huyo anaweza kutolewa kwenye urithi, lakini Bwana

8 Anna ni sarafu ya zamani nchini India iliyo sehemu ya 16 ya rupia. (mfasiri)

Sayyid katika kila hali amezipoteza kabisa haki za mmliki, na hii ni dhulma kubwa.

Na kuhusu kipimo cha maelezo ya Kurani Tukufu ambacho Bwana Sayyid amemwuliza rafikiye mpinzani, nimeona yafaa hapo pia mimi mwenyewe nimtolee huduma hii Bwana Sayyid, kwani kumwongoza njia aliyepotea ni jukumu langu kwanza kuliko wengine wote. Hivyo inapaswa kufahamu ya kwamba:

**Kipimo cha kwanza** kabisa cha maelezo sahihi ya Kurani Tukufu ni shuhuda za Kurani Tukufu. Yafaa jambo hili likumbukwe vizuri sana kwamba Kurani Tukufu si kama vitabu vingine vya kawaida inayomhitaji mwingine kwa kuthibitisha kweli zake au kuzidhihirisha. Ni kama jengo lenye uwiano mmoja ambalo kama tofali lake moja tu litingishwe basi umbo zima la jengo laharibika. Hakuna ukweli wake wowote ule usiokuwa na angalau shuhuda kumi au ishirini mumo humo. Basi tukitoa tafsiri fulani ya aya fulani ya Kurani Tukufu, tunapaswa tutazame kwamba je, zapatikana shuhuda zingine ndani ya Kurani Tukufu ili kusadikisha tafsiri hiyo au la? Ikiwa shuhuda zingine haipatikani, bali shuhuda zipatikanazo zinapingana wazi kabisa na aya zingine zenye maana hizo, basi tunapaswa tufahamu kuwa tafsiri hiyo ni batili kabisa, kwani

haiwezekani kwamba kuwe na hitilafu ndani ya Kurani Tukufu; na alama ya tafsiri za kweli ni hii tu kwamba kuwepo ndani ya Kurani Tukufu jeshi la shuhuda bayana kwa kuisadikisha.

**Kipimo cha pili** ni maelezo ya Mjumbe wa Mungu s.a.w. Hamna shaka kwamba mwenye kuzielewa zaidi maana za Kurani Tukufu alikuwa ni mpenzi wetu na nabii wetu mtukufu, Hadhrat Rasulullahi s.a.w., hivyo maelezo yakithibitika kutoka kwa Mtume s.a.w., ni faradhi ya Mwislamu kuyakubali bila kusita wala wasiwasi, au la ndani mwake mtakuwa na mwelekeo wa ukafiri wa ufalsafa.

**Kipimo cha tatu** ni maelezo ya Masahaba r.a. Hamna shaka yoyote katika jambo hili kwamba Masahaba r.a. walikuwa wenye kupata nuru za Mtume s.a.w. na walikuwa warithi wa kwanza wa elimu ya unabii, na fadhili kubwa ya Mwenyezi Mungu ililkuwa juu yao na msaada wa Mwenyezi Mungu ulikuwa pamoja na nguvu yao ya ufahamu kwa sababu wao hawakuwa tu wasemaji, bali na watekelezaji pia.

**Kipimo cha nne** ni kuitafakari Kurani ukiwa na nafsi yako iliyotakaswa, kwani Kurani Tukufu inalingana na nafsi iliyotakaswa. Mungu Mwenye shani tukufu Anasema:

لَا يَمَسُّهٗٓ اِلَّا الْمُطَهَّرُوْنَ ۝٨٠ [9]

Yaani, kweli za Kurani Tukufu hufuguliwa kwa wale tu wenye mioyo iliyotakasika, kwani kwa mwanadamu mwenye moyo uliotakasika maarifa matakatifu ya Kurani Tukufu hufunguliwa kutokana na ulingano alionao (na Kurani) naye huyatambua na kuyanusa, na moyo wake husema: Naam, hii ndiyo njia ya kweli; na nuru yake ya moyo huwa kipimo bora cha kupimia. Hivyo, maadamu mtu si mtambuzi hasa na si mwenye kupita njia ile nyembamba waliyopita manabii a.s., basi inafaa asijifanye mfasiri wa Kurani akikosa adabu na akijivuna; la sivyo maelezo yake yatakuwa rai tu yake, jambo ambalo Nabii a.s. alilikataza na akasema:

مَنْ فَسَّرَ الْقُرْآنَ بِرَأْيِهٖ فَاَصَابَ فَقَدْ اَخْطَأَ

Yaani, yule aliyeeleza Kurani kwa kutumia tu rai yake na akadhani kuwa ameeleza vizuri, hata hivyo ameeleza vibaya.

**Kipimo cha tano** ni lugha pia ya Kiarabu. Lakini Kurani Tukufu yenyewe imekwisha stawisha njia zake kiasi hiki hata kwamba hakuna haja ya kufanya sana utafiti wa kamusi za Kiarabu; naam, bila shaka huo huwa sababu ya kuongeza busara, bali wakati mwingine kwa kuchunguza lugha huibuka mwelekeo

9 Hapana atakayeigusa ila waliotakaswa. Al-Waaqi’a : 80

wa kuelekea kwenye siri zilizojificha za Kurani Tukufu na jambo fulani la siri hutokeza.

**Kipimo cha sita** cha kuufahamu mfumo wa kiroho ni mfumo wa kimwili; upo uwiano mkamilifu baina ya mifumo miwili ya Mwenyezi Mungu.

**Kipimo cha saba** ni wahyi wa Uwalii na kashfi za Wahaddithiina.[10] Na kipimo hiki kinajikusanyia

10 Bwana Sayyid, ndani ya kitabu chake chochote hakuukiri wahyi kuwa ni kipimo cha ukweli na wala hataki kukiri hivyo. Sababu yake inavyoonekana ni kwamba yeye hauthamini wahyi uwe wa Unabii au wa Uwalii, bali anaufikiria kuwa ni kipawa tu cha asili; hivyo kuhusu rai yake hii inafaa hapa kuielezea. Basi, ibainike kuwa rai hii ya Bwana Sayyid ya kudhani kwamba wahyi wa Mwenyezi Mungu ni kipawa tu anachokimiliki mtu ni rai batili kabisa na yenye kuzaa fitina na yenye kupeleka mbali na ukweli. Jambo hili ni dhahiri kuwa ndani ya asili ya mwanadamu mna vipawa vya aina mbalimbali, na vipawa vyote ni hivi kwamba namna na sura ya kimoja hushuhudia kwa namna na sura ya kingine. Kwa mfano, tabia ya asili ya baadhi yao hulingana na elimu ya hesabati na jiometri, na baadhi yao na elimu ya utabibu na ya baadhi wengine na elimu ya mantiki na theolojia. Lakini vipawa hivyo vilivyofichikana haviwezi vyenyewe kumfanya mtu awe mtaalamu wa hesabati na mhandisi au tabibu au mwanamantiki; bali mtu huyo huwa anamhitaji mwalimu. Na halafu mwalimu mwenye busara aionapo tabia ya asili ya huyo mtu kulingana na elimu fulani makhsus, basi humshawishi kuisoma elimu hiyo. Ubeti huu unaeleza habari hiyo:

vipimo vingine vyote, kwa sababu yule apataye wahyi wa kimuhaddath yuafanana kabisa na Nabii anayemfuata, naye hupewa mambo yote yale

---

Humfanyiza kila mmoja kwa kazi fulani, na humwekea ndani mwake maelekeo ya tabia yake kwenye kazi hiyo.

Baada ya kupata elimu hii, kipawa kile kimejificha kama mbegu huwaka, naye anapata kugundua sehemu nyepesi za namna namna za elimu hiyo. Na mambo yote mapya mapya yahusikanayo na fani hii yanayozalika moyoni mwake toka kwa Mwenyezi Mungu, yakiitwa Ilham (ufunuo) na Ilqaa (kutilia moyoni na Mungu) si mbali na uhakika, kwa sababu bila shaka mambo yote mazuri yawafaayo wanadamu huwa yanatiliwa moyoni toka kwa Mwenyezi Mungu, kama vile Mwenyezi Mungu Mwenye shani pia kwa hakika Akiashiria kwenye jambo hili hili Asemavyo:

فَأَلْهَمَهَا فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا ۝٩

(Kisha Akaifunulia maovu yake na wema wake. Ash-Shams: 9) Yaani mambo mabaya na mambo mema yaingiayo nyoyoni mwa wanadamu huwa ni Ilhaam kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mtu mwema kutokana na tabia yake njema anastahili kuwa mambo mema yaingie moyoni mwake; na mtu mbaya kutokana na tabia yake mbaya anastahili kwamba mawazo mabaya na mashauri mabovu yaendelee kuzalika moyoni mwake. Na kwa hakika mtu mwema, kwa kupata Ilhaam za aina hii, anacho kitabia kipawa cha wema ndani yake, na mtu mbaya kitabia ana kipawa cha uovu. Hivyo kutokana na kipawa hiki hiki cha asili watu wengi wameacha kumbukumbu yao ya maandiko mema na mabaya na maneno safi na machafu. Lakini swali ni hili kwamba je, uhakika

aliyopewa Nabii isipokuwa Unabii na sheria mpya, naye kwa yakini kabisa hudhihirishiwa elimu ya kweli; na sio kiasi hicho tu, bali hujaaliwa yote kama

---

wa wahyi wa manabii pia ni huu tu kwamba huo nao kwa hakika ni kipawa tu cha asili ambacho chanufaika na ile hali ya kutiliwa fikara moyoni za aina ambazo maelezo yake yametolewa sasa hivi? Ikiwa ni hivyo tu, basi hakika imekwisha julikana! Kwani kwa kuuchukua wahyi wa manabii kuwa kipawa tu cha asili; inakuwa vigumu sana kupambanua kati ya manabii na watu wengine wa aina hii. Labda hapo Bwana Sayyid atasema kwamba sisi twakubali wahyi utamkwao, yaani Kurani Tukufu kuwa ni maneno yaliyo wahyi. Lakini mimi naielewa vema hila ya Bwana Sayyid. Yeye kamwe haukiri huu wahyi ulio na maneno maalumu kama tunavyokiri sisi. Ni dhahiri kwamba fikira inayotiliwa moyoni haiwi hivi hivi tu bila ya maneno; na maana hizo zisizo na maneno haziwezi asilani kuingia akilini. Lakini pia kuna tofauti moja baina ya Kurani na Hadithi za Mtume s.a.w., na kwa sababu ya tofauti hiyo hatuhesabu maneno ya Hadithi kuwa yametoka kwenye chemchemi ile yalikotokea maneno ya Kurani, ingawa kwa kuzingatia maana ya kawaida ya Ilqaa (kutiliwa moyoni na Mungu) na Ilhaam (ufunuo) maneno ya Hadithi pia ni ya kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwani aya isemayo:

وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوٰى ۝ اِنْ هُوَ اِلَّا وَحْيٌ يُّوْحٰى ۝

(Wala hasemi kwa tamaa(Ya nafasi yake). Siyo haya ila ni ufunuo uliofunuliwa. An-Najm : 4)

inatoa ushahidi wa hilo. Twalikumbuka tena jambo hili kuwa Ilqaa ya aina yoyote ile daima itaambatana na maneno. Kwa mfano, mshairi atafutaye mstari wa pili wa ubeti unaolingana na ule wa

neema na kwa heshima anayojaaliwa Nabii anayemfuata. Hivyo, maelezo yake yanakuwa siyo ya kubahatisha, bali anasema baada ya kuona na anatamka baada ya kusikia, na njia hii ipo wazi kwa

---

kwanza, atakapopata Ilqaa toka kwa Mwenyezi Mungu, hiyo itakuwa imeambatana na maneno.

Sasa, kwa kuwa imekwisha amuliwa kwa imara kuwa wanafalsafa na wenye maarifa na washairi pia hupata Ilqaa toka kwa Mwenyezi Mungu tu nayo pia huwa ni Ilhaam yenye maneno, na miongoni mwao walio wakweli hupewa kipawa cha ukweli na walio wabaya hupewa kipawa cha uovu, na kulingana na kipawa hicho huwa wanaendelea kupata Ilhaam, kwa mfano yule aliyevumbua garimoshi naye alipata Ilqaa na yule aliyevumbua telegramu pia katika maana hiyo alikuwa ni mwenye kupata Ilhaam, hapo ukinzani ule ule tuliokwisha taja utamkabili Bwana Sayyid. Kama Bwana Sayyid akijibu kwamba kwa hakika katika Ilqaa yenyewe manabii na wanafalsafa, bali na kafiri na mwaminio, wote ni sawa lakini tofauti ni hii kwamba Ilqaa ya manabii daima huwa sahihi, basi kwa jibu hili Bwana Sayyid atalazimika kukubali kuwa wahyi wa unabii hauna tofauti yoyote ya dhati na ilhaam za makafiri ila tu jambo lililozidi ni kwamba wahyi wa manabii huwa hauna makosa na wahyi wa aikna Aristotle, Plato na wanafalsafa wengineo haukuepuka makosa. Lakini madai haya hayana uhakikisho, bali ni kutumia tu nguvu, kwa sababu hapo tunalazimika kuamini kuwa sehemu ile kubwa ya mawaidha, nasaha na maneno ya khulka njema ya wanafalsafa ambayo haina makosa na yaafikiana na Kurani Tukufu, ndiyo bila shaka yoyote neno la Mungu na kuihesabu kuwa sawasawa na Kurani Tukufu na kuiamini kuwa ni

umati huu. Haiwezekani hata kidogo pasiwepo na mrithi wa kweli na kwamba yule mtu ambaye ni mdudu wa ardhini aliyenaswa katika heshima,

---

maneno maalum yaliyofunuliwa; na shehemu nyingine ambamo mna makosa ndani yake tuiingize ndani ya makosa ya Ijtihadi kama manabii pia wanavyopata kufanya makosa ya Ijtihadi; na ndiyo kulingana na kanuni hii wanafalsafa hao bali hata makafiri pia tuwafahamu kuwa manabii.

Sasa ni dhahiri kwamba, kwa hakika, hili ni wazo ambalo kwalo ni karibu imani ya Bwana Sayyid ipotee, bali huenda wakati fulani akaja kuufahamu wahyi wa wanafalsafa kama vile Newton kuwa bora zaidi kuliko wahyi wa Kurani. Ole! Laiti kama Bwana Sayyid angeichukua Kurani yenyewe kuwa kipimo cha kuielewa maana ya Kurani basi angesalimika kuangukia shimo hili la maangamizi. Kurani haikutoa popote mfano wa wahyi wake kwamba ni kama chemchemi ile ibubujikayo ardhini, bali kila mahali imejifananisha na mvua inyeshayo toka mbinguni. Na kama Bwana Sayyid, wakati wa kuandika angemwuliza mjuzi wa habari hii kwamba wahyi wa Mwenyezi Mungu ni kitu gani na huteremkaje, hapo pia angeepuka kuteleza huko. Kwa kujikwaa huko, Bwana Sayyid amewaangamiza idadi kubwa ya Waislamu na kuwafikishia karibu na ukafiri na udaharia na akiondoa heshima ya wahyi wa Unabii kwa kuuwekea mipaka ya kipawa cha asili ambamo hata makafiri na wasio na imani hushiriki.

Wakati huu natoa ushahidi wangu kwa Bwana Sayyid kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, asaa Mwenyezi Mungu akamjalia fadhili. Hivyo, ewe azizi Bwana Sayyid! Naapa kwa Mungu Mwenye

adhama na staha za dunia, huyo ndiye awe mrithi wa elimu ya unabii, kwani Mwenyezi Mungu Ameishaahidi kwamba elimu ya unabii hatapewa

---

shani tukufu, kwamba ni sahihi kwa hakika kwamba wahyi huangukia moyoni toka mbinguni kama mwonzi wa jua ukutani. Mimi huona kila siku kwamba ufikapo wakati wa kuongea na Mwenyezi Mungu kwanza mara moja huwa natawaliwa na hali iliyo baina ya kulala na kuamka, na hapo mimi huwa kama kitu kilichobadilika, na ingawa hisia zangu, utambuzi na ufahamu wangu hubakia kidhahiri lakini wakati huo mimi hujikuta kana kwamba Dhati fulani Mwenye nguvu kubwa sana Amenishika mwili wangu mzima mkononi mwake na hapo najihisi kwamba mishipa yote ya uhai wangu imo mkononi mwake na chote kilicho changu si changu tena bali ni chake. Itokeapo hali hii, hapo kwanza kabisa Mwenyezi Mungu Huweka mbele yangu mawazo ya moyoni ambayo Anaridhia kuyatupia mwonzi wa maneno Yake. Ndipo kwa namna ya ajabu mawazo hayo huja mbele yangu moja baada ya jingine, na inakuwa hivi kwamba wazo fulani, kwa mfano, kumhusu Zaid limekuja moyoni kuwa yeye atapona au hatapona maradhi fulani basi mara moja kipande cha ufunuo wa Mwenyezi Mungu huliangukia kama mwonzi, na mara nyingi mwili mzima hutetemeka kwa kuanguka kwake. Halafu baada ya kuamuliwa kesi hiyo wazo lingine hujitokeza. Na wazo hilo likijitokeza tu mbele ya macho, papo hapo kipande cha ufunuo huliangukia kama vile ambavyo mwindaji aendelea kulitupia mshale kila windo litokapo. Na wakati huo twahisi kuwa mlolongo huu wa mawazo huzalika kutokana na kipawa chetu cha asili na maneno yaangukayo juu yake huteremka toka juu. Ingawa washairi na kadhalika pia hupata *ilkaa* baada ya kutafakari, lakini

yeyote isipokuwa wale waliotakaswa; bali huku ni kuichezea elimu hii takatifu kwamba kila mtu, juu ya kuwa na hali yake chafu, adai kuwa mrithi wa Nabii.

---

kuilinganisha na wahyi huo ni utovu mkubwa wa adabu, kwa sababu *ilkaa* hiyo ni matokeo ya kufikiri na kutafakari na hudhihiri katika hali ya mtu kujitambua na kuwa katika mipaka ya ubinadamu. Lakini *ilkaa* hii hutokea wakati ule tu mwanadamu anaposhikwa na Mwenyezi Mungu kikamilifu, hajitambui kabisa wala hahusikani na fikara zake kwa namna yoyote; wakati huo ulimi huonekana kama kwamba si wake bali nguvu nyingine kubwa sana inautumia. Na kutokana na sura hii niliyoielezea inafahamika kwa uwazi kabisa kuwa utaratibu wa kipawa cha asili ni kitu gani na ni nini kiteremkacho toka mbinguni. Mwishoni naomba dua kwamba Mwenyezi Mungu Afutilie mbali mioyoni mwa Waislamu itikadi hii yenye nuhusi katika kanuni ya asili hata kwamba kusibakie doa lake kabisa ndani yake, kwani jicho lolote linalozitazama baraka za Islam haliwezi kufunguka maadamu moshi huu hautatoweka na kupotelea mbali.

(Tafsiri ya beti za Kiajemi)

1. *Ee kanuni ya asili uliye mtundu! ni udhia gani huu, kwa mkono wako fitina zimezuka kila upande.*
2. *Yule aliyeipenda njia yako potovu, hakushika tena njia iliyonyoka.*
3. *Lakini nifikiripo, naona msiba wetu huu umesababishwa na sisi wenyewe.*
4. *Tangu Kurani imeachwa kusomwa, mabalaa yamefanya mashambulizi.*
5. *Tabia ya asili haikuwa yenyewe mbaya, lakini nuru ya akili ikapungua kwa sababu ya dini kupotea.*

Na huu pia ni ujahili wa hali ya juu kabisa kwamba ikataliwe kuwepo kwa wale warithi na ishikwe itikadi kuwa sasa siri za unabii zapaswa kuchukuliwa kuwa kisa kilichopita, ambazo hazipo mbele ya macho yetu na wala hakuna uwezekano wake, na wala haupo mfano wake wowote. Sivyo hivyo; kwani, kama ingekuwa hivyo, Islam isingeweza kuitwa dini iliyo hai, bali ingekuwa pia dini iliyokufa kama dini zingine, na katika hali hii itikadi kuhusu unabii nayo ingekuwa ni kisa tu ambayo ingekuwa inarejeshwa kwenye karne zilizopita. Lakini Mwenyezi Mungu Hakupenda hivyo, kwa sababu Yeye Alikuwa Anajua

---

6. *Watu wakaelekea mara moja kwenye tone la maji, wakaupa kisogo upande ulioelekea mto.*
7. *Wanaicheka imani katika Pepo na ufufuo, wakisema habari hii iko mbali sana na akili.*
8. *Malaika wapatapo kutajwa, husema habari hii ni kunyume na akili ya wenye busara.*
9. *Ewe Sayyid uliye kiongozi wa kaumu hii, zinduka, kwani mguu wako.*
10. *Ukafikiriaje uzeeni! Nenda ukatubu; njia hii siyo ya ucha-Mungu.*
11. *Nachelea, siku moja utasema kwa kubahatisha hivyo kwamba kuwepo kwa Mungu ni wazo lisilo sawa*
12. *Ee Bwana! jitenge na fikara hizo, kwani kutia fikara ya binadamu katika kazi ya Mungu ni namna moja ya umajinuni.*
13. *Kwa vyovyote, kubahatisha kwafaaje? Kaa tu, huku siko mahali pa kupayuka na kupiga kelele.*
14. *Ee mja! jitakie busara kwa Mungu; siri za Mungu siyo mali ya mateka!*

vyema kuwa uthibitisho wa uhai wa Islam na uhakika wa kweli wa unabii uwezao daima kila zama kuwanyamazisha wakataaji wa wahyi waweza kustawi katika hali hii tu kwamba kufunuliwa wahyi katika sura ya kimuhaddath kuendelee daima. Basi, Akafanya hivyo hivyo. Muhaddathina ni watu ambao wamepewa heshima ya kuongea na Mwenyezi Mungu na asili ya nafsi zao inafanana sana na asili ya nafsi za manabii. Na sifa hizo za ajabu huwa alama zilizobakia za Unabii ili habari hii nyepesi ya kushuka wahyi isije katika zama zozote ikawa ni kisa tu ikikosa uthibitisho. Na wazo hili si sahihi hata kidogo kwamba manabii walipita duniani bila ya kuacha warithi, na sasa kudhihirisha rai yoyote kuhusiana nao haina thamani yoyote zaidi ya masimulizi ya visa. Bali katika kila karne waliendelea kuzaliwa warithi wao kulingana na mahitaji, na katika karne hii ndimi mimi. Mwenyezi Mungu Amenituma kwa ajili ya kuzirekebisha zama hizi, ili makosa yale yasiyoweza kuondolewa bila msaada makhsus wa Mwenyezi Mungu yaondolewe toka katika mawazo ya Waislamu, na wakanaji wapewe uthibitisho wa Mungu wa kweli na Aliye hai, na taadhima na ukweli wa Islam uthibitishwe kwa ishara zilizo mpya. Na ndicho hicho hicho kinachotokea. Maarifa ya Kurani Tukufu yanadhihirika, maana nyepesi na za ndani kabisa za maneno ya Mwenyezi Mungu zinafunguka,

ishara za kimbingu na miujiza inatokea, na Mwenyezi Mungu Anaonyesha upya dhihirisho la uzuri, nuru na baraka za Islam. Mwenye macho ya kuona na atazame, na mwenye jazba ya kweli na atamani, na aliye na chembe ya penzi la Mwenyezi Mungu na Mtume s.a.w. ainuke na kujaribu na ajiunge katika Jumuiya hii ya Mwenyezi Mungu Aipendayo ambayo tofali lake la msingi Aliliweka kwa Mkono Wake Mtakatifu. Na kusema kwamba njia ya kupata wahyi wa Unabii sasa imefungwa na ishara haziwezi kudhihirika na dua hazikubaliwi, hiyo ni njia ya maangamio siyo ya usalama. Msizikatae fadhili za Mwenyezi Mungu. Inukeni mkajaribu na kupima, halafu mkinikuta kuwa ni mtu mwenye ufahamu wa kawaida, akili ya kawaida na maneno ya kawaida, basi msikubali. Lakini kama muone dhihirisho la Kudra na muukute mng'ao wa Mkono ulioendelea kudhihiri kwa waliosaidiwa na Mungu na wale ambao Mwenyezi Mungu Alisema nao, basi mkubali. Na fahamuni kwa yakini kwamba hisani kubwa kabisa ya Mwenyezi Mungu kwa waja Wake ni hii tu kwamba Yeye Hataki kuifanya Islam kuwa dini iliyokufa, bali daima Anataka kuziweka wazi njia za yakini, maarifa na kumsuta mbishi. Hebu, wenyewe fikirieni kwamba kama kuna mtu aukataaye wahyi wa Unabii na aseme kwamba wazo hilo ni dhana tupu tu yenu, hapo yawezekana dalili gani ya kumfumba midomo yake

minghairi ya kumuonyesha mifano yake? Je, hii hii ni habari njema au habari mbaya kwamba baraka za kimbingu zikae ndani ya Islam kwa miaka michache tu halafu ikawa dini kavu na iliyokufa? Na je, hizo ndizo alama zinazostahili kuwa za dini ya haki?

Ilmuradi, hivyo ndivyo vipimo kwa ajili ya maelezo sahihi ya Kurani. Na hamna shaka yoyote kwamba katika sehemu nyingi ya maelezo (ya Kurani) ya Bwana Sayyid mmekosekana vipimo hivyo saba na siyo makusudio yetu wakati huu kushughulikia habari hii. Bwana Sayyid alikuwa anaringa sana kwa kanuni ya tabia ya asili, lakini ndani ya maelezo yake ya Kurani hakuijali kanuni hiyo ya maumbile. Kwa mfano, itikadi yake hii kwamba wahyi wa Unabii si kitu chochote zaidi ya kuwa kipawa tu cha tabia ya asili ya mtu, na kati yake na Mwenyezi Mungu hamna mawasiliano ya Malaika, inapingana sana namna gani na kanuni ya asili iliyowekwa na Mwenyezi Mungu. Tunaona wazi kabisa kuwa kwa kukamilisha nguvu zetu za kimwili twahitaji njia ya kimbingu. Kwa kustawisha utaratibu huu wa kimwili na kwa kuufikisha kwenye malengo yanayotakiwa, Mwenyezi Mungu Ametutiishia jua, mwezi, nyota, na elementi, na baada ya kupitia kwenye njia za aina nyingi neema za Mungu hutufikia, na katu hazifiki moja kwa moja. Kwa mfano, ingawa macho yetu

hupata nuru toka kwa Mwenyezi Mungu, kwani Yu Sababu ya sababu zote, lakini Yeye Hufikisha hiyo kwenye macho yetu kwa njia ya jua. Hatuoni kitu chochote katika mfumo wa kidhahiri ambacho Mwenyezi Mungu Mwenyewe Anatupatia moja kwa moja kwa kunyosha Mkono wake wenye baraka; bali kila kitu twakipata kwa kupitia njia fulani. Halafu pia tunaona kwamba umbile la nguvu zetu za kidhahiri si kamilifu; yaani haziko hivi kwamba, kwa mfano, zing'arike kwa kujitegemea na kiwemo humo kipawa, kama vile kipawa cha wahyi sawa na mawazo yako, ambacho kitufanye tusiwe na haja ya jua. Basi kauli zako zisizo na msingi dhidi ya mfumo huu zinawezaje kuwa sahihi. Mbali na hayo, ushahidi wa tajiriba za binafsi ambao unazishinda shuhuda zote unaikadhibisha vikali rai yako hii, kwa sababu tangu miaka kumi na mmoja mimi nimejaaliwa heshima ya kuongea na Mwenyezi Mungu na jambo hili nalifahamu vyema kuwa wahyi kwa hakika huteremka tu toka mbinguni. Mfano wa wahyi kama utolewe kwa kitu chochote cha duniani, basi labda kwa kiasi fulani unafanana na telegramu, ambao hutoa habari ya kila badiliko lake. Mimi nimeshuhudia kwamba wakati wa kupata wahyi unaonishukia kwa sura ya Wahyi wa Uwalii, nahisi nimetawaliwa toka nje na athari yenye nguvu, na pengine kutawaliwa huku kunakuwa na nguvu kubwa

hata kwamba kunanibana ndani ya nuru zake, nami najiona nimevutwa upande wake kwa namna ambavyo hakuna nguvu yangu yoyote iwezayo kukabiliana nayo. Katika hali hii ya kutawaliwa huwa nasikia maneno maalum wazi wazi yang'aayo. Wakati mwingine mimi nawaona Malaika[11] na ninashuhudia ile athari na heba ambayo huwa ndani ya ukweli, na mara nyingi maneno hayo yanaeleza habari za ghaibu; na kutawaliwa huku na kushikwa huku huwa kutoka nje ambako huthibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Sasa kuikana hiyo ndiyo kuukataa katakata ukweli ulio wazi.

Inafaa kwamba Bwana Sayyid aukubali ukweli huu leo kabla ya kufa na asiudharau wahyi utokao mbinguni. Ni ajabu kwamba anaiona nidhamu ya dhahiri lakini hailinganishi na nidhamu ya batini. Hafahamu kwamba Yule Mungu Aliyeifanya nidhamu yetu ya kimwili hivi kwamba nuru ya dhahiri inateremka toka mbinguni kwa ajili yetu, na Mtoa athari wa kweli Huteremsha baraka Zake juu ya nguvu zetu za kimwili kwa kutumia njia za kimbingu. Na kuteremsha baraka yoyote bila ya kutumia sababu za kati siyo desturi yake hata kidogo, hivyo iweje

---

11 Siyo tu kwamba malaika huonekana baadhi ya wakati, bali wakati mwingine hudhihirisha kwamba wao ndio njia ya kati kufunuliwa maneno ya wahyi.

Mungu Huyo katika nidhamu yetu ya kiroho Atutenge kabisa na mfumo wa kutumia njia za kati! Je, tumetengwa na mfumo huu kimwili au kwa hakika tumefungwa ndani ya mfumo wa njia za kati ambao huanzia toka kwa Sababu ya sababu zote na kutufikia sisi. Kwa kuzingatia maelezo haya yafaa kuvipitia vitabu vyetu *'Taudhihi Maraam'* na *'Aina Kamalate Islam'*; hususan kuhusu haja ya kuwepo kwa Malaika maelezo kwa mapana na marefu yametolewa ndani ya *'Aina Kamalate Islam'* hata kwamba hamwezi kukuta mfano wake ndani ya kitabu kingine chochote. Kwa kuelewa kadiri Bwana Sayyid anavyomjua Mungu zinatosha kauli zake hizi ya kwamba yeye amewafanya viumbe wasimhitaji Mweka Kudura wa kweli madaraka Yake na enzi Zake. Haelewi kuwa Uungu wa Mwenyezi Mungu umeambatana na Kudra yake kamilifu, na kudra ndiyo hii kwamba saa zote madaraka Yake juu ya viumbe vyake yasiwe na mpaka. Bila shaka hii ni kweli kwamba ikiwa Yeye Ndiye Aliyeviumba hivyo viumbe, basi kama ambavyo dhati Yake haina mipaka vivyo hivyo hakuna budi kwamba alikwisha jiwekea nafasi ya madaraka yake yasiyo na mipaka ili katika daraja lolote lile Uungu wake usilazimike kukomeka.[12] Na

12 Ikiwa shutuma hii itolewe kwamba kwa kuamini jambo hili kuwa hekima isiyo na kikomo ya Mwenyezi Mungu inao uwezo

ikiwa, Mungu Apishe mbali, kauli za Mabaniani wa Kiaria ni sahihi ya kwamba Mungu si Mwumbaji wa kila chembe ya ulimwengu, hapo bila shaka Mungu

---

wa kugeuza vitu katika sura nyingi mbalimbali zisizo na kikomo, hakika za vitu hazitaaminika. Kwa mfano, ikiwa Mwenyezi Mungu Afahamike kuwa mwenye uwezo wa kutowesha sura asilia ya maji na kuyawekea sura ya hewa, au kuondoa sura ya asili ya hewa na badala yake kuiwekea sura ya asili ya moto, au kuuondolea moto sura yake ya asili na kuupa sura asilia ya maji kutokana na sababu zile zilizofichikana Azijuazo, au kuugeuza udongo kuwa dhahabu katika tabaka fulani ya ardhi kwa kuuletea mabadiliko mepesi, au kuigeuza dhahabu kuwa udongo, hapo amani itatoweka na elimu na fani zitapotea, basi jibu la swali hili ni kwamba wazo hili ni batili kabisa; kwani twaona kwamba Mwenyezi Mungu kwa kutumia hekima Zake zilizofichikana Huleta mabadiliko ya mamia ya aina mbalimbali kwa elementi na kadhalika. Itazame tu ardhi yenyewe kwamba inageuka kuwa nini na nini kwa mabadiliko ya aina mbalimbali. Mumo humo hutokea sumu ya kiaseni (Arsenic) na humo humo hutokea tiba ya sumu (Bezoar), na humo humo dhahabu na humo humo fedha na humo humo aina mbalimbali za vito hutokea. Kadhalika upandapo mvuke, vitu vya aina ngapi vinazalika angani. Toka katika mvuke huo huo theluji hudondoka, na kutoka huo mvua ya mawe hutokea, na toka huo huo umeme na toka huo huo mngurumo hutokea; na hii pia imethibitika kuwa wakati mwingine hata majivu huanguka toka angani. Je, elimu hubatilika kutokana na hali hizo au amani hutoweka? Na kama mkisema kwamba Mwenyezi Mungu, tangu mwanzo, Ameviwekea vitu hivyo sifa ya mabadiliko haya yote, basi jibu letu litakuwa kwamba ni lini na wakati gani tuliposema

mnyonge kiasi hicho atakoma baada ya kuwa na utawala dhaifu kwa muda na atakashifiwa kwa fedheha. Lakini Mungu wetu Mweza si hivyo. Yu

---

kuwa ndani ya vitu hivyo tunavyovijadili haijawekwa sifa hiyo ipatikanayo katika vyote hivyo. Bali itikadi iliyo sahihi na ya kweli ndiyo hii kwamba Mwenyezi Mungu Aliye Mmoja katika dhati Yake, Ameviumba vitu vyote kama kitu kimoja ili vidokeze kwenye Umoja wa Mwumbaji Mmoja. Basi, Mwenyezi Mungu kwa asili ya Umoja huu huu na kwa sababu ya uwezo Wake usio na mpaka Ameviwekea sifa ya kubadilika badilika. Na kwa kuacha roho zile ambazo bahati zao njema na mbaya zimezifanya kudumu katika hali zao na ahadi ya Mwenyezi Mungu imeziwekea umbo usiobadilika, chochote kingine miongoni mwa viumbe hakionekani kuwa kimeepukana na mabadiliko. Bali kama mkiona kwa makini mtakuta kwamba kila wakati ndani ya kila mwili badiliko latokea, hata kwamba utafiti wa elimu ya fizikia umethibitisha kuwa hadi miaka mitatu mwili wa binadamu hubadilika na mwili wa awali hutoweka ukiwa chemchembe. Kwa mfano, kama ni maji ama ni moto, hivyo navyo havijakosa mabadiliko; na aina mbili za mabadiliko huvitawala. Moja ni kwamba baadhi ya sehemu hutoka na baadhi ya sehemu mpya huja kuungana. Pili ni kwamba zile sehemu zinazotoka, hizo huchukua umbile lingine sawa na viwango vyao. Ilmuradi, kuiweka daima dunia hii ya kupita juu ya kapi la mabadiliko ni sunna ya Mwenyezi Mungu. Na kwa kuangalia kwa makini sana inafahamika kwamba vitu vyote hivi, kwa sababu ya chanzo kimoja cha baraka, ni vimoja katika asili zao ingawa mtengenezaji wa vitu hivi hawezi kuwa binadamu, na anawezaje kuwa hivyo kwani Mwenye Hekima tupu Hakumjaalia yeyote mwingine kutambua kikamilifu siri

Muumbaji wa chembe zote za ulimwengu na roho na viumbe vyote. Kuhusu uwezo wake kama iulizwe, basi ifahamike kwamba kwa kuacha yale mambo

---

za hekima zake zisizo na kikomo. Na kama ukisema mabadiliko ya wapi katika vitu vya angani (jua, mwezi, sayari n.k.), basi mimi nasema kwamba bila shaka hata humo pia mna sifa za kubadilika na kugeuka hata kama tusijue, ndiyo sababu siku moja zitachakaa. Isitoshe, baada ya kuyashuhudia mabadiliko ndani ya maelfu ya vitu, yathibitika kuwa hakuna kitu chochote kile chenye kukosa mabadiliko. Basi, kataeni kwanza mabadiliko ya ardhini halafu ndio muongelee mambo ya angani.

*Je, umekwisha tengeneza tayari kazi ya ardhi,*
*hata washughulikia pia mbingu.*

lmuradi, kila siku tunaposhuhudia aina mbalimbali za mabadiliko, na yaonekana ni lazima kwa Umoja wa Dhati kwamba chimbuko na chanzo cha vitu vyote hivi kiwe kimoja, na pia Uungu kamili wa Mwenyezi Mungu waweza kuimarika hapo tu ambapo Yeye Awe na mamlaka kamili juu ya kila chembe, hapo kuifikiri kuwa ni kinyume na akili na kuleta shutuma hii kwamba kwa mabadiliko hayo amani itatoweka na elimu zitapotea, kama si kosa kubwa ni nini tena? Na tusemapo kwamba Mwenyezi Mungu Mwenye Shani tukufu ni Mwenye uwezo wa kuufanya moto ufanye kazi ya maji, au maji yafanye kazi ya moto, haina maana kwamba Afanye hivyo bila kutumia hekima Yake isiyo na kikomo na afanye hivyo kwa kutumia nguvu tu, kwa sababu kitendo chochote cha Mwenyezi Mungu hakiko bila kuwa na hekima ndani yake na wala hakipaswi kuwa hivyo. Bali twamaanisha kwamba wakati Atakapo kuifanya kazi ya moto kwa (kutumia) maji au kazi ya maji kwa (kutumia) moto, basi hapo Ataumia hekima ile inayotawala kila

makhsus yanayopingana na sifa zake zilizokamilika na ahadi zake za kweli, Yeye anao uwezo juu ya mambo yote. Na kusema kwamba ingawa yeye ni

---

chembe ya ulimwengu huu hata kama twaifahamu au la. Ni dhahiri kwamba kazi ifanyikayo kwa hekima haipotezi elimu, bali kwayo elimu hupata maendeleo zaidi. Hebu tazameni, maji hugeuzwa kuwa barafu, au mwanga wa umeme unatengenezwa; je, kwa sababu hiyo amani inatoweka au elimu zinapotea?

Hapa pana siri nyingine inayostahili kukumbukwa, nayo ni kwamba pengine miujiza ya aina hii hutokea kwa Mawalii kwamba maji hayawezi kuwazamisha na moto hauwezi kuwadhuru. Humo pia, kwa hakika, kuna siri hii hii kwamba Mwenye Hekima tupu Ambaye mwanadamu hawezi kuzitambua siri zake zisizo na kikomo, pengine Huonyesha onyesho la nguvu yake wakati wa mwelekeo wa marafiki Zake na waja Wake waliomkurubia kwamba mwelekeo huo unaleta mabadiliko katika ulimwengu, na kwa kujumuika kwa zile sababu zilizofichikana, kwa mfano, joto la moto laweza kusitishika kuathiri hata kama sababu hizo ziwe ni athari za vitu vya angani au iwe, kwa mfano, sifa fulani ya moto iliyofichikana, au sifa fulani ya mwili wake (mja wa Mungu) iliyofichikana, au uwe mjumuiko wa sifa zote hizo, basi sababu hizo zaanza kufanya kazi kutokana na mwelekeo huo na dua hiyo. Hapo jambo fulani kinyume na kawaida hudhihirika, lakini kwa sababu hiyo imani juu ya hakika za vitu haitoweki wala elimu hazipotei; bali hiyo yenyewe ni elimu mojawapo kati ya elimu za kiungu, na ipo kwenye mahali pake, na kanuni ya moto kuunguza, kwa mfano, ipo mahali pake. Bali fahamuni kwamba hizo ni maada za kiroho ambazo zikiushinda

Mwenye uwezo lakini hataki kufanya, hiyo ni shutuma ya ajabu ya kivoloya ambapo ndani ya sifa zake pia mna:

---

moto zinaonyesha athari zake na zinahusikana na wakati wake na mahali pake. Akili ya kidunia haiwezi kulifahamu jambo hili jepesi kwamba mwanadamu mkamilifu anakuwa ni mahali pa dhihirisho la roho ya Mwenyezi Mungu. Na kila umfikiapo mtu mkamilifu wakati ambapo ndipo wakati hasa wa mdhihirisho huo, hapo kila kitu kinamwogopa kama kimwogopavyo Mungu. Wakati huo umtupe mbele ya mnyama mbuai, umtumbukize motoni, yeye hawezi kudhurika navyo hata kidogo, kwani wakati huo roho ya Mwenyezi Mungu huwa juu yake, na ni ahadi ya kila kitu kumuogopa. Hii ndiyo siri ya mwisho ya maarifa amabyo haiwezi kufahamika bila ya kukaa pamoja na waja wakamilifu. Kwa kuwa hili ni jambo jepesi sana na tena hutokea kwa nadra mno, hivyo kila akili haina habari ya falsafa hii. Lakini kumbukeni kwamba kila kitu kinaisikia sauti ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Anayo mamlaka juu ya kila kitu, na nyugwe zote za kila kitu zimo mkononi mwa Mwenyezi Mungu. Hekima Yake ni hekima isiyo na kikomo ambayo imefika kwenye chimbuko la kila chembe. Na ndani ya kila kitu mna sifa kadiri zilivyo kudra zake. Yule asiyeamini jambo hili, mtu huyo yumo katika kundi la walioelezwa hali yao katika:

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ

(Na hawamheshimu Mwenyezi Mungu kama inavyotakiwa kumheshimu. Al-Anaam : 92).

Na kwa kuwa mtu mkamilifu huwa dhihirisho timilifu la ulimwengu mzima, hivyo ulimwengu wote huwa unavutiwa kwake mara kwa mara. Yeye huwa ni buibui wa ulimwengu wa

كُلَّ يَوۡمٍ هُوَ فِي شَأۡنٖ ۝٢٩ [13]

Na madaraka yake ya kuondoa ubaridi toka kwenye maji au kutokomeza sifa ya kuunguza toka kwenye moto si kinyume na sifa zake zilizokamilika na ahadi zake za kweli, basi kwa nini tena inasemwa kwa kutumia nguvu kwamba Amelazimika kwa kudumu Asilete mabadiliko katika sifa za vitu hivyo. Kuna dalili ipi ya ulazima huu na kuna sababu gani? Na Mwenyezi Mungu ana haja gani ya kulazimika huko bila sababu ambako kunatia hata doa kwenye Uungu Wake. Inaonekana kwamba ndani ya kijitabu hicho Bwana Sayyid pia amefahamu ubovu wa wazo hilo dhaifu, ndiyo sababu kwa ajili ya kuibeba kauli yake mbovu ametoa udhuru mwingine mbovu nao ndio kwamba katika mahali fulani ndani ya Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu Ameashiria kuwa moto ni wenye kuunguza na mahali pengine Amedokeza kuwa maji ni yenye baridi, na wakati mwingine Amesema kuwa jua kutoka mashariki huelekea magharibi. Hayo maneno yaliyo kwa ajili ya kueleza hali zilivyo hivi sasa katika fikara ya Bwana Sayyid ni kama ahadi

---

kiroho na ulimwengu mzima ni nyuzi zake, na hiyo ndiyo siri ya miujiza ionekanayo kuwa kinyume na kanuni ya asili.

(Tafsiri ya ubeti wa Kiajemi)

*Katika shuguli za dunia hii kuna athari ya waja wa*
*Mungu; asiyeitazama hiyo, ameitazama nini ya dunia hii?*

13 Kila siku Yeye anakuwa katika shani. Ar-Rahmaan :30

ambazo haziwezi kugeuka wala kubadilika. Ikiwa hiyo ndiyo njia ya kuleta hoja, basi Bwana Sayyid atapata matatizo makubwa na atalazimika kuamini kuwa maelezo yote ya Kurani Tukufu ndiyo ahadi. Kwa mfano Mwenyezi Mungu Akimpa Hadhrat Zakaria habari njema Aliposema: إِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلَٰمٍ[14]

Kwa mujibu wa kanuni ya Bwana Sayyid ilipaswa kwamba Hadhrat Yahya angelidumu kuwa kijana kwa sababu Mwenyezi Mungu Alimwita Hadhrat Yahya kuwa ni 'Ghulam,' na hiyo ikawa ahadi. Kuna mifano maishirini ya aina hii, kuieleza yote ni kupoteza tu wakati. Ikiwa katika fikira ya Bwana Sayyid, kwa kueleza matukio ya sasa hivi hulazimika kufanyika ahadi kwa siku zijazo na kwa kudumu milele, basi yapasa kumhofia, kwani kwa njia hiyo atawasingizia wanadamu kwa kila jambo, likielezwa tukio fulani la sasa atalifahamu hilo kuwa ni ahadi ya milele. Nafikiri, ni afadhali kwamba Bwana Sayyid akiikumbuka siku yake ya mwisho akae nami kwa miezi michache. Na kwa kuwa mimi nimetumwa na ni mwenye kutoa habari njema, kwa hiyo ninaahidi kwamba kwa kumtuliza Bwana Sayyid nitamwelekea Mungu, nami nina matumaini kuwa Mwenyezi Mungu Ataonyesha ishara yoyote ambayo mara moja itaisambaratisha mavumbini kanuni ya maumbile

14 Hakika Tunakupa habari njema ya mtoto. Maryam : 8

iliyopendekezwa na Bwana Sayyid. Na mambo mengi kama hayo yameshatokea hadi sasa ambayo kwa maoni ya Bwana Sayyid yanapingana na kanuni ya maumbile, lakini kuyaelezea hakuna faida yoyote kwa kuwa Bwana Sayyid atayafikiria ni kisa tu. Bwana Sayyid anakanusha hata zile bishara za wahyi wa Uwalii ambazo Mawalii wa Mwenyezi Mungu wanapata kujua kwa njia ya ufunuo; katika maoni yake hizo zapingana na kanuni ya maumbile kama vile moto kuacha ile sifa yake ya kuunguza. Vivyo hivyo athari binafsi za dua ambazo kwazo yale makusudio hupatikana yaliyoombewa dua, hizo zinapingana na kanuni ya maumbile machoni mwa Bwana Sayyid. Hivyo, kama Bwana Sayyid hawezi kuja kwangu, basi katika mambo hayo mawili, akitoa ahadi ya kuukubali ukweli, aniruhusu nimuelekee Mwenyezi Mungu kwa maombi na nichapishe yatakayonidhihirikia. Kwayo watu wote watafaidika. Ikiwa rai ya Bwana Sayyid kwa hakika ni sahihi, basi sitofanikiwa katika matashi yangu, waila watu wenye akili baada ya kuepuka itikadi mbovu za Bwana Sayyid watamfahamu Mwenyezi Mungu Mwenye shani kubwa na kurejea Kwake kwa mapenzi, na wakati wa kuomba dua hawatakuwa wenye kukata tamaa ya rehema Zake, na watapata ladha wanyanyuapo mikono. Na faida ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu ndiyo hii kwamba Asikilize dua

zetu na Atupashe habari ya kuwepo Kwake; siyo kwamba kwa kupata shida maelfu kwa maelfu tuimarishe moyoni mungu wa bandia kama sanamu, ambaye hatuwezi kusikia sauti yake na wala hatuwezi kuona onyesho la kudra yake iliyo wazi. Fahamuni kwa yakini kuwa Mungu Mweza Yupo Aliye na uwezo juu ya kila kitu. Mikono yake haikufumba, bali mikono yake miwili imefumbuka, Hutoa jinsi Apendavyo na Hufanya Atakayo, naye Anao uwezo juu ya kila kitu. Na mwito wetu wa mwisho ni kwamba sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu.

(Tafsiri ya shairi la Kiajemi)

1. *Uso wa Mpendwa haukufichikana kwa watafutao. Huo ndio ung'aao katika jua na pia mwezini.*
2. *Lakini uso huo mzuri umefichikana kwa walioghafilika. Mwenye kupenda anatakiwa kuwepo ili kwa ajili yake kifuniko cha uso kiondolewe*
3. *Huwezi kumpata Mtakatifu Huyo kwa kiburi, kwa ajili yake hakuna njia isipokuwa unyenyekevu na kiherehere.*
4. *Njia ya kuelekea mtaa wa Mpenzi huyo Asiye na mwanzo ni ya hatari; ukitaka*

*usalama na uhai wako, uachane na njia ya majivuno.*

5. *Fahamu na akili ya wasiostahiki haiwezi kufikia maana ya ndani ya Maneno Yake; kila atenganaye na majivuno, ndiye apataye njia iliyo sawa.*
6. *Mafumbo ya Kurani hayawezi kufumbuliwa na wana-dunia; yule tu aijua ladha ya mvinyo hiyo aiinywaye.*
7. *Ewe usiye na habari yoyote ya nuru za batini, lolote utuambialo halitukasirishi.*
8. *Tumesema hayo kwa nasaha na huruma, ili jeraha hilo baya lipate kupona kwa marahamu hii.*
9. *Uyatibu maradhi ya kukana dua kwa dua, kama kitibiwavyo kileo kwa kileo wakati wa kulewa chakari.*
10. *Ewe usemaye kwamba kama dua zina athari basi hiyo athari iko wapi, nikimbilie haraka nikakuonyeshe hiyo athari kama jua.*
11. *Naam, usikatae siri hizi za kudra ya Mungu. Katiza maneno, shuhudia kwetu dua ikubaliwayo.*

# Habari nyingine kumhusu Lekh-Ramu wa Peshawar.

Leo tarehe 2 April, 1893 sambamba na tarehe 14 ya mwezi wa Ramadhani mwaka 1310 Hijiria, majira ya asubuhi, niliona nikiwa katika hali baina ya kulala na kuamka kwamba nimekaa ndani ya nyumba moja yenye wasaa na marafiki wachache pia wapo pamoja nami, mara mtu mmoja aliye pande la mtu, mwenye sura ya kutisha, kana kwamba ameghadhibika vikali sana sana, akaja na kusimama mbele yangu. Nikainua macho na kumtazama, nikafahamu kuwa yeye ni mtu wa umbo na tabia ngeni, kana kwamba si mwanadamu bali ni miongoni mwa Malaika wakali wenye nguvu; na nyoyo zilitishika kwa hofu yake. Nilipomtazama tu akaniuliza Lekh-Ramu yuko wapi? Na akataja jina la mtu mwingine kuwa yu wapi? Ndipo nikafahamu wakati huo kuwa huyo ametumwa kwa kuwaadhibu Lekh-Ramu na yule mtu mwingine, lakini sikumfahamu yule mtu wa pili ni nani. Naam nakumbuka kwa yakini kabisa kuwa yule mtu wa pili alikuwa miongoni mwa wale watu wachache ambao kuwahusu hao nimekwisha tangaza. Na hiyo ilikuwa siku ya Jumapili, majira ya saa kumi za usiku. Basi, alhamdulillahi kwa hayo.

**Isomeni kwa makini,**

**kwani humu mna habari njema kwa ajili yenu.**

## Kwa maamiri na watemi na matajiri wenye uwezo na viongozi wa serikali na wenye vyeo.

بِسۡمِ اللّٰهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِيۡمِ [15]

نَحۡمَدُهٗ وَ نُصَلِّی عَلٰی رَسُوۡلِهِ الۡکَرِيۡمِ [16]

Enyi wazee wa Kiislamu! Mwenyezi Mungu Awajaalie mioyoni mwenu dhamira njema kuliko makundi mengine yote na Akufanyeni muwe wahudumu wa kweli wa dini yenu kipenzi. Wakati huu kwa ajili tu ya Mwenyezi Mungu nawajulisha kuwa Mungu Amenituma kutoka Kwake, mwanzoni mwa karne hii ya kumi na nne kwa kuijadidisha na kuisaidia dini hii imara ya Islam ili katika zama hizi za machafuko nidhihirishe mazuri ya Kurani na taadhima za Mtume s.a.w. na kwa msaada wa nuru na baraka na miujiza na elimu zitokazo Kwake

15 Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

16 Twamsifu Yeye, na Twamsalia Mtume wake mhashamu.

nilizojaaliwa niwajibu maadui wote wale wanaoishambulia Islam. Basi kazi hii inaendelea kufanyika tangu miaka kumi mfululizo. Lakini kwa kuwa vifaa vyote tunavyohitaji kwa kueneza Uislamu vinataka misaada mingi ya mali, kwa hiyo nimeonelea hakuna budi niwajulisheni kwa njia ya mahubiri. Hivyo, sikilizeni enyi wenye jaha kubwa, tunayo matatizo katika njia ya Mwenyezi Mungu na Mtume s.a.w. kwamba kwa vitabu vinavyopaswa vienezwe baina ya malaki ya watu yahitajika rasilmali nyingi sana. Na hivi sasa, hali ni hii kwamba kwanza kwa ajili ya malengo haya makubwa makubwa hakuna rasilmali yoyote; na kama kitabu chochote baada ya kutungwa kichapwe kwa hima na msaada wa baadhi ya watu wa dini[17] wenye jazba, basi kwa sababu ya watu kutokujali sana na kughafilika kitabu hicho hakipati kuuzwa isipokuwa nakala chache na nakala zake nyingi ama hufungiwa ndani ya masanduku kwa miaka na miaka au hutolewa bure kwa lilahi na kwa njia hii uenezaji wa mambo ya

17 Hapo watu wa dini wenye jazba muradi wake ni ndugu yangu Hadhrat Maulawii Hakim Nuruddin wa Bhera ambaye ametoa, yaonekana, mali yake yote katika njia hii. Na baada yake ni rafiki yangu wa kweli Bwana Hakim Fadhluddin na Bwana Nawab Muhammad Ali Khan wa Kotla Malir na daraja kwa daraja wale marafiki wote waaminifu wanaojitolea mhanga katika njia hii. Mwandishi.

muhimu ya dini unapata madhara sana. Na ingawa Mwenyezi Mungu Anaendelea kuipanua Jumuiya hii siku hadi siku, lakini mpaka sasa kutoka miongoni mwa matajiri hamna hata mmoja pamoja nasi ambaye aweze kubeba jukumu la sehemu kubwa ya huduma hii ya Islam. Na kwa kuwa mimi nimetumwa na Mwenyezi Mungu kuja kuijadidisha dini na Mwenyezi Mungu Amenipa bishara hii njema kwamba Atawaingiza ndani ya kundi letu baadhi ya matajiri na wafalme na Ameniambia: Nitakupa baraka juu ya baraka hadi wafalme watatafuta baraka toka kwenye nguo zako, basi kwa sababu hiyo limenijia wazo leo kwamba niwahimize matajiri na wenye uwezo kuisaidia kazi yangu.

Na kwa kuwa kazi hii ya kuisaidia dini ni kazi adhimu sana, na mwanadamu hakuepukana na shuku, mashaka na wasiwasi na bila ya utambuzi hauzaliki ukweli ule uwezao kuhamasisha kutoa misaada mikubwa, basi waniandikie baadhi ya makusudio yao na mambo yao muhimu na matatizo ili niombe dua ya kutimia kwa makusudio hayo; lakini itabidi waandike kwa uwazi kabisa kuwa wakati yatimiapo matashi yao watatuletea kiasi gani cha msaada wa mali katika njia ya Islam, na kwamba je, wamekwisha funga ahadi imara na madhubuti mioyoni mwao kwamba

lazima watatoa msaada kiasi hicho. Ikinifikia barua[18] ya aina hiyo toka kwa mtu yeyote yule, basi nitamuombea dua, nami nina yakini kwamba kama siyo kadiri isiyotanguka, basi lazima Mwenyezi Mungu Atayasikia maombi yangu na Atanijulisha kwa njia ya ufunuo. Msikate tamaa kuwa makusudio yetu ni tata mno, kwani Mwenyezi Mungu Ana uwezo juu ya kila kitu kwa sharti kwamba isiende kinyume na dhamira Yake ya tokea azali. Na kama yaje maombi mengi sana ya watu hao, hapo watajulishwa ambao nitakuwa nimepata bishara njema toka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye Heshima na Ujalai, kuhusu utatuzi (wa makusudio yao). Na mambo haya yatakuwa pia ni ishara kwa wale wenye kukataa; na huenda ishara hizi zikawa nyingi hata kwamba zianze kutiririka kama mto. Mwishoni ninasema kwa kumnasihi kila Mwislamu kwamba amkeni kwa ajili ya Islam, kwani Islam imo ndani ya shida kubwa. Isaidieni, kwani kwa sasa i masikini, nami nimekuja kwa sababu hii hii, na Mwenyezi Mungu Amenijaalia elimu ya Kurani na Amenipa miujiza. Hivyo, njooni kwangu ili nanyi pia mpate

---

18 Inatakiwa barua iletwe kwa uangalifu sana iliyopigwa muhuri, kwa rejista na siri ile isifichuliwe mapema; na hapa pia siri ile itatunzwa kwa uaminifu mkamilifu. Na kama badala ya barua aje mtu mwaminifu kutoka Amiri yeyote basi jambo hili litafaa zaidi. Mwandishi.

hisa katika neema hii. Ninaapa kwa Yule ambaye nafsi yangu imo mkononi Mwake kwamba mimi nimetumwa toka kwa Mwenyezi Mungu. Je, haikulazimika kwamba mwanzoni mwa karne kama hii yenye fitina nyingi kubwa, ambayo maafa yake ya wazi kabisa, aje Mujaddidi na madai yaliyo wazi kabisa? Basi, hivi karibuni mtanitambua kwa kazi yangu. Kila aliyekuja toka kwa Mwenyezi Mungu ukosefu wa ufahamu wa wanazuoni wa zama hizo ukawa kikwazo kwake. Na hatimaye alipotambulika alitambulika kutokana na kazi yake, kwani mti mchungu hauwezi kuleta matunda matamu. Na Mwenyezi Mungu huwa Hawapi wengine baraka zile Awapazo waja Wake makhsus. Enyi watu! Islam imekuwa dhaifu mno na maadui wa dini wameihusuru pande zote nne, na jumla ya shutuma zimekuwa zaidi ya elfu tatu. Katika wakati kama huu onyesheni imani yenu kwa huruma mkapate kuingia miongoni mwa waja wa Mungu. Na amani iwe juu ya yule afuataye mwongozo.

(Tafsiri ya shairi la Kiajemi)

1. *Dini ya Ahmad s.a.w. imekuwa haina msaidizi; hakuna aliye rafiki yake. Kila mtu yumo katika shughuli zake, haijali dini ya Ahmad s.a.w.*

2. *Mafuriko ya upotevu yamechukua malaki ya wanadamu na kutupa kila upande. Ole wake jicho lisilozinduka hata sasa.*
3. *Enyi wenye mali, kwa nini mwaghafilika kiasi hiki? Je, mmelala fofofo, ama bahati ya dini imekwisha lala?*
4. *Enyi Waislamu, tupeni jicho kwenye hali ya dini hata mara moja. Mabalaa niyaonayo, hamna haja kuyaeleza.*
5. *Enyi wanaume, inukeni; nguo zake zimeshika moto! Si kazi ya wenye dini kuiangalia toka mbali !!*
6. *Moyo wangu kila saa unafurukuta katika damu; hakuna ayajuaye maumivu yetu minghairi ya Mjuzi wa siri.*
7. *Huzuni tunayoipata hakuna aijuaye isipokuwa Mungu. Twainywa sumu, lakini hatuna uwezo wa kusema.*
8. *Kila mmoja anawahurumia ahali na jamaa zake, lakini ni masikitiko, dini isiyo na msaidizi haina wa kuihurumia !!*
9. *Naona damu ya dini ikitiririka kama waliouawa huko Karbalaa. Ni ajabu kuwa watu hawa hawana huba ya Mpenzi huyu!*
10. *Nashangaa nionapo kutumia mali nyingi kwa mambo yao ya binafsi kwani huo ukarimu unakosekana katika njia ya Mungu.*

11. *Ewe uliye na uwezo na pia wanuia kuisaidia dini, toa tu, hatujali watoa kidogo au nyingi.*
12. *Tazama jinsi dini isiyo na kifani chini ya mbingu inavyogaragara vumbini kwa kudhulimiwa na watu waovu.*
13. *Katika wakati wa msiba huu, sisi wanyonge hatuna tiba isipokuwa dua ya asubuhi na kulia saa za kabla ya kupambazuka.*
14. *Ee Mungu, Usiufurahishe ule moyo wenye giza usiojali dini ya Ahmad Mteule s.a.w.*
15. *Ee ndugu, siku za anasa ni chache sana, raha na ustawi wa bustani haudumu milele.*

Mwandishi,
Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian,
Wilaya ya Gurdaspur, Panjab.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ [19]

اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَّ اٰلِ مُحَمَّدٍ اَفْضَلِ الرُّسُلِ وَ خَاتَمِ النَّبِيِّيْنَ [20]

# Tangazo

Kitabu cha Barahine Ahmadiyya ambacho mwandishi baada ya kufunuliwa na kutumwa na Mwenyezi Mungu ameandika kwa makusudio ya kuisuluhisha na kuijadidisha dini, ambacho pamoja nacho kuna tangazo la rupia elfu kumi ambalo muhtasari wa muradi wake ni kwamba humu duniani dini iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu, iliyo ya kweli, ambayo kwayo mwanadamu akimtambua Mwenyezi Mungu kuwa Ameepukana na kila aibu na kasoro, anaziamini kwa yakini ya moyo sifa Zake zote takatifu zilizokamilika, ndiyo Islam pekee, ambamo baraka za ukweli zinameta kama jua, na nuru ya ukweli inadhihirika kama mchana. Na dini zingine zote ni batili kwa uwazi hata kwamba kwa utafiti wa kiakili misingi yake haithibitiki kuwa sahihi au sawa, na wala haiwezekani kupatikana hata chembe baraka ya kiroho na ukubaliko wa Mungu kwa kuzifuata hizo, bali kwa kushikamana nazo mwanadamu anakuwa

---

19 Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

20 Ee Allah, msalie Muhammad na ali zake Muhammad, Mbora wa Mitume na Muhuri wa Manabii.

hana busara na anakuwa mwenye moyo mweusi ambaye alama za yeye kuwa mwenye bahati mbaya huzalika hapa hapa duniani:

Ndani ya kitabu hicho ukweli wa dini ya Kiislamu umethibitishwa kwa namna mbili: (1) kwanza: kwa dalili mia tatu za kiakili zilizo madhubuti na zenye nguvu ambazo shani yake na thamani yake ni dhahiri kwa jambo hili kwamba kama mpinzani yeyote wa Islam apate kuzivunja dalili hizo basi limekwisha tolewa tangazo la kumpatia huyo rupia elfu kumi. Kama yeyote anataka, anaweza pia kusajilisha mahakamani kwa kujihakikishia; (2) pili, kwa zile ishara za kimbinguni ambazo ni za lazima kwa ajili ya kuthibitisha ukweli kamili wa dini ya kweli. Katika suala hili la pili, mwandishi, kwa lengo hili kwamba ukweli wa dini ya Islam ung'ae kama jua, amethibitisha aina tatu za ishara. Kwanza ni zile ishara ambazo wapinzani walizishuhudia katika zama za Mtume s.a.w. zikidhihirika kwa mkono wake Mtukufu (s.a.w.) kutokana na dua, mwelekeo na baraka zake ambzo mimi mwandishi nimeziandika ndani ya kitabu kwa uthibitisho makhsus na wa hali ya juu ulio bayana, utokanao na historia. Pili ni zile ishara zipatikanazo ndani ya Kurani yenyewe yenye baraka kwa kudumu milele kwa namna zisizo kifani, ambazo nimezifafanua kwa maelezo bayana na toshelevu kwa watu wote wala sikumwachia yeyote nafasi ya udhuru wa aina yoyote ile. Tatu, ni zile ishara

azipatazo mtu kama urithi kwa sababu ya kukifuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kumfuata Mtume wa haki s.a.w., ambazo kwa fadhili za Allah Mweza, mimi mtumishi wa kizingiti cha Mungu nimeonyesha thibitisho zake kwa uwazi kabisa kwamba Ilham nyingi za kweli, dua zilizokubalika nilizoomba mimi mtumishi wa dini na ambazo ukweli wake umeshuhudiwa na kuonwa na wapinzani wengi wa dini yetu (Wa-Ariya n.k) zimeandikwa ndani ya kitabu kilichotajwa. Na mwandishi wa hicho kitabu amepewa elimu ya jambo hili kwamba yeye ndiye Mujaddidi wa zama hizi, na sifa zake bora kiroho zinafanana na sifa bora za Masihi, mwana wa Mariamu, nao wanalandana na kushabihiana sana; na kama walivyo manabii na mitume makhsus, yeye (mwandishi) kwa baraka tu za kumfuata mheshimiwa aliye mbora wa viumbe na mbora wa mitume, s.a.w., amepewa fadhila juu ya wengi wa hao mawalii wakubwa waliopita kabla yake. Na kufuata nyayo zake ni sababu ya kupata wokovu, bahati njema na baraka; na kwenda kinyume naye ni sababu ya kwenda mbali na Mungu na kujinyima. Thibitisho zote hizi zinadhihirika kwa kusoma kitabu cha Barahine Ahmadiyya ambacho kwa jumla kina kurasa 1200 ambamo karibu kurasa 148 zimeshachapishwa. Na kwa kutuliza na kumwondolea shaka mtafuta haki, mwandishi mwenyewe wa kitabu yupo na yuko tayari kila wakati. Na hiyo ni fadhili ya Mwenyezi Mungu Humpa Amtakaye wala siyo fahari; na

amani iwe juu ya yule aufuataye mwongozo. Na ikiwa hata baada ya tangazo hili, mtu akiwa mtafuta haki wa kweli hataki kutatuliwa utata wake na hahudhurii kwa moyo wa kweli basi sisi tutakuwa tumeshamtimizia hoja ambayo atalazimika kuijibu mbele ya Mwenyezi Mungu. Mwishoni tangazo hili lamaliziwa kwa dua hii kwamba: Ewe Mwenyezi Mungu, Uwajaalie mwongozo watu wenye kujitahidi wa kaumu zote ili wamwamini Mtume Wako mwenye kukubalika na aliye mbora wa mitume, Muhammad Mustafa s.a.w., maneno yako matakatifu, Kurani Tukufu, na watekeleze maamrisho yake ili wanufaike na zile baraka zote na wawe wote na hali njema za kweli ambazo Waislamu wa kweli huzipata duniani na akhera, na wawe wenye mafanikio katika wokovu wa daima na maisha ya milele na ambavyo si tu vyaweza kupatikana huko Akhera, bali watu wema wa kweli huvipata katika dunia hii hii. Na hasa kaumu ya Waingereza amabo hadi sasa hawajapata mwanga wowote wa jua hili la ukweli, na ambao serikali yao adibu, iliyostaarabika na yenye huruma kwa kutufanyia hisani na kututendea kirafiki imetutilia moyoni jazba kwamba tuwatakie, kwa shauku ya moyo, ustawi na usalama katika dunia yao na dini yao, ili nyuso zao nyeupe jinsi zilivyo nzuri hapa duniani, huko Akhera pia ziwe zenye nuru na kunawirishwa. Basi twamwomba Mungu heri yao duniani na huko Akhera. Ee Mungu, waongoze na wasaidie kwa roho kutoka kwako, na Uwajaalie hadhi nyingi katika dini

Yako na Uwavutie kwa uwezo Wako na nguvu Yako ili waamini Kitabu Chako na Mtume Wako s.a.w. na waingie katika dini ya Mungu makundi kwa makundi. Amina thumma Amina. Na sifa zote njema ni za Mungu, Mola wa walimwengu.

Mtangazaji,
Mnyenyekevu,
Mirza Ghulam Ahamd kutoka Qadian,
Wilaya ya Gurdaspur, Panjab.